# YALIYOMO

UTANGULIZI .......................................................................... 1

VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KATIKA BAJETI YA MWAKA 2016/17 .......................................................................... 7

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17 .......................................... 10

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17 .......................................... 13

A: AFYA .......................................................................... 13

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya .......................................... 13

Huduma za Kinga .......................................................................... 17

Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko .............................................. 17

Udhibiti wa Malaria .......................................................................... 19

Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma .............................................. 21

Udhibiti wa UKIMWI .......................................................................... 23

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele .... 27

Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto .............................................. 27

Huduma za Chanjo .......................................................................... 33

Usafi wa Mazingira .......................................................................... 35

Elimu ya Afya kwa Umma .......... 38
Huduma za Lishe .......... 39
Huduma za Tiba .......... 41
Huduma za Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda .......... 41
Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Tiba Nchini .......... 51
Huduma za Matibabu kwa Wazee .......... 53
Huduma za uchunguzi .......... 54
Huduma za Damu Salama .......... 57
Huduma za kinywa .......... 57
Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala .......... 59
Huduma za Dawa .......... 59
Huduma za Uuguzi Na Ukunga .......... 63
Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya .......... 63
Uratibu, Ufuatiliaji na Ugharamiaji Huduma za Afya .......... 69
Uratibu na Ufuatiliaji Huduma za Afya .......... 69
Ugharamiaji wa Huduma za Afya .......... 72
Udhibiti wa Kemikali Nchini .......... 77
Udhibiti wa Ubora wa Chakula, Dawa, Vipodozi na Vifaa Tiba .......... 79
Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu .......... 81



B: MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO .......... 83
Maendeleo ya Jamii .......... 83
Vyuo vya Maendeleo ya Jamii .......... 84
Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi .......... 85
Maendeleo ya Jinsia .......... 87
Ukatili wa Kijinsia .......... 89
Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi .......... 89
Maendeleo ya Watoto .......... 92
Maendeleo na Ustawi wa Wazee .......... 95
Ustawi wa Jamii .......... 96
Taasisi ya Ustawi wa Jamii .......... 99
Mashirika yasiyo ya Kiserikali .......... 99
Uratibu wa Sera, Programu na Mipango ya Wizara .......... 101
Ushirikiano wa Ndani na Nje ya Nchi .......... 102
SHUKRANI .......... 103
MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17 .......... 110
VIREFU VYA VIFUPISHO .......... 114
VIAMBATISHO .......... 122
Kiambatisho Na.1: Vituo vinavyotoa huduma za uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya Saratani ya mlango wa kizazi .......... 122

Kiambatisho Na.2: Mgawanyo wa majokofu, masanduku ya baridi, baiskeli na vifaa vya kuhifadhia chanjo ..................... 125

Kiambatisho Na.3: Mgawanyo wa virutubishi vinavyowekwa katika unga wa mahindi katika Halmashauri sita za majaribio ............................................................................ 128

Kiambatisho Na. 4: Vituo vilivyofanyiwa Tathmini kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card) mwaka 2015/16 129

Kiambatisho Na 5: Wanufaika wa Huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) 2012-13 hadi 2015-16 (Disemba) ................................................ 131

Kiambatisho Na 6: Mchanganuo wa Fedha zilizolipwa na NHIF kwa Watoa Huduma .......................................................... 132

Kiambatisho Na 7: Takwimu za Wataalam wa Maendeleo ya Jamii Katika Halmashauri Kufikia Machi, 2016 ..................... 133

Kiambatisho Na. 8 Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Katika Wilaya na Mikoa.......................................................................... 148

Kiambatisho Na. 9 Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Katika Wilaya na Mikoa ................................................................ 149

Kiambatisho Na. 10 Takwimu Za Ukatili Wa Kijinsia Januari - Disemba 2015..................................................................... 153

Kiambatisho Na. 11 Hali ya Uchangiaji wa Baadhi ya Halmashauri Kwenye Mfuko wa WDF .................................. 156

Kiambatisho Na.12 Idadi ya Mabaraza ya Watoto Hadi Machi, 2016 ................................................................................. 159

Kiambatisho Na.13 Mchanganuo wa Idadi ya NGOs Zilizosajiliwa na Kupata Cheti cha Ukubalifu Kuanzia Januari Hadi 31 Machi, 2016........................................................... 167



# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17

## UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2015/16 na Mipango ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa mwaka 2016/17.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunikabidhi majukumu ya kusimamia Wizara hii. Wajibu ulio mbele yangu ni kukidhi matarajio yake na matarajio ya Watanzania kwa kufanya kazi kwa kasi na ufanisi mkubwa ili kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma bora za afya na kujenga jamii inayojali usawa wa jinsia pamoja na kuimarisha haki za wazee na watoto. Aidha, namshukuru na kumpongeza pia kwa uongozi wake imara na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na kuimarisha huduma za Afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto. **Mheshimiwa Rais** amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa huduma za afya na usafi wa mazingira zinaboreshwa. Vilevile, **Mheshimiwa Rais** ametoa kipaumbele kwa kuweka misingi inayowezesha kusimamia na kuendeleza haki za makundi maalum ikiwemo haki ya watoto kupata elimu kupitia mpango wake wa elimu bure ngazi ya msingi na sekondari. Kwa jinsi hiyo Wizara itaendelea kuelimisha na kuhimiza umma wa Watanzania kuhusu usafi wa mazingira, haki za wazee na watoto.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati katika kuboresha



huduma za Afya hasa afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Akiwa ndiyo Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Tanzania, Wizara yangu itaendelea kutumia taswira, ushawishi na uzoefu wake ili kujenga jamii ya watanzania inayowajali kuwaheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana kwa ajili ya kuwa na maendeleo ya kweli endelevu katika nchi yetu

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara yangu. Aidha, naomba nimpongeze kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge hili ambayo ni dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2016/17.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inadhihirisha jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyo na imani kubwa kwako katika kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson**

**Mwansasu (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kuaminiwa kuwa sehemu ya uongozi wa Bunge hasa katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nimshukuru **Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb)** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na **Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Pia, nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb)**, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, namshukuru Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto **Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel (Mb)** kwa ushirikiano mkubwa anaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hotuba zilizotangulia. Michango yao imesaidia kuboresha hotuba yangu. Nawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na ninaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.



8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali. Ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendelee kuwatumikia wananchi kwa pamoja. Aidha napenda kuwapongeza Wabunge wote kwa kuaminiwa na wananchi katika majimbo yao. Ni Imani yangu kuwa watatimiza wajibu wao kikamilifu kwa wapiga kura wao ambao wengi ni wanawake.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali. Vilevile, natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka, ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo ya vipaumbele vya Wizara katika bajeti ya 2016/17 pamoja na utekelezaji wa kazi za wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/17.



## VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KATIKA BAJETI YA MWAKA 2016/17

11. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika bajeti ya mwaka 2016/17 ni kama ifuatavyo:

    i. Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, kuongeza usawa katika utoaji wa huduma za afya na kupunguza vifo vya wanawake wajawazito,

    ii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya,

    iii. Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu,

    iv. Kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC, Mbeya na Mtwara.

    v. Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya,

vi. Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya,

vii. Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya.

viii. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Afya.

ix. Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojiunga na Mifuko ya Bima za Afya.

x. Kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto ikiwemo kupambana na mimba na ndoa za utotoni;

xi. Kuimarisha na kupanua juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuhamasisha uanzishwaji wa SACCOS na VICOBA vya wanawake, kuwapatia elimu ya ujasiriamali, biashara na kuwaunganisha na vyombo vya fedha ikiwemo Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake;

xii. kuimarisha miundombinu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi ili kuwapatia maarifa na stadi za kuwajengea uwezo wa kujitegemea na kuinua hali za maisha yao na taifa kwa ujumla



xiii. Kuwajengea uwezo watumishi wa maendeleo ya jamii wa Halmashauri ili kuchochea ari na mwamko wa wananchi wa kutumia rasilimali zilizopo katika kuongeza kipato kwa jamii hasa vijana na wanawake;

xiv. Kuimarisha haki, ulinzi na usalama wa wazee pamoja na kukarabati makazi ya wazee, shule za maadilisho na mahabusi za watoto na kuwapatia chakula; na

xv. Kuwezesha mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazokinzana na haki za wanawake na watoto ambazo ni: Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sura ya 29 na marekebisho yake ya mwaka 2002; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004; Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009; na Kanuni za Mirathi Na. 279 za mwaka 1963

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17

### Mapato na Matumizi ya Fedha

### Fungu 52 - Afya

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kupitia Fungu 52 (Afya) hukusanya mapato yake kupitia Bodi na Mabaraza mbalimbali, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 87,117,583,604** ikilinganishwa na makadirio ya **Shilingi 122,998,941,500.00** yaliyoidhinishwa kwa mwaka 2015/16. Hii ni asilimia **70.8** ya makadirio ya makusanyo ambayo yamevuka lengo kutokana na usimamizi thabiti na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kukusanya **Shilingi 163,755,679,857.00.**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, jumla ya **Shilingi 780,740,723,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo,



**Shilingi 340,098,271,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 440,642,452,000.00** za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2016 jumla ya **Shilingi 604,547,066,537.00** zilipokelewa ikiwa ni **asilimia 77.4** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 269,205,005,123.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 335,342,061,414.00** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Vilevile, kati ya fedha zilizopokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo kiasi cha **Shilingi 309,409,703,350.00** ni thamani ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyo pokelewa kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

### Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara yangu kupitia Fungu 53, iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo na shabaha zilizopangwa. Katika bajeti ya mwaka huo, Wizara ilitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 2,712,550,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 27,501,007,000** ambapo kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi**

**18,627,587,000** yakijumuisha **Shilingi 11,038,075,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 7,589,512,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ni **Shilingi 8,873,420,000**

***15.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2016, makusanyo yalifikia **Shilingi 1,815,145,600** sawa na **asilimia 66.9** ya lengo. Fedha za Matumizi Mengineyo **Shilingi 3,870,651,121** zilipokelewa sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 4,138,691,435** za Mishahara zilipokelewa sawa na **asilimia 37** ya bajeti iliyoidhinishwa. Vilevile, bajeti ya miradi ya Maendeleo, **Shilingi 827,087,080** fedha za nje sawa na **asilimia 28** ya fedha za nje zilizoidhinishwa zilipokelewa.



## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17

### A: AFYA

***16.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inazingatia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2016 -2020) na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007 – 2017). Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

***17.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ifuatayo ni taarifa ya sekta ya afya ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 na mpango wa mwaka 2016/17.

### RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

***18.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa kuongeza idadi ya

wanafunzi watarajali wa ngazi ya kati waliodahiliwa katika vyuo vya Afya na kufikia **11,192** kwa mwaka. Hivyo, kuvuka lengo la kudahili wanafunzi **10,000** kwa mwaka waliolengwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017. Aidha, Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi **295**, wanaochukua mafunzo ya uzamili katika vyuo mbalimbali ya ndani (**275**) na nje (**20**) ya nchi, lengo ni kufadhili wanafunzi 350.

***19.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2015/16, Wizara imepunguza pengo la upungufu wa watumishi kutoka asilimia 58 mwaka 2011/12 hadi kufikia asilimia 51 mwaka 2015/16. Hii imetokana na utekelezaji wa Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa. Aidha, Wizara imeongeza uwiano wa kitaifa kati ya madaktari na watu wanowahudumia, kutoka Madaktari **7.74** mwaka 2014/15 hadi **9.03** mwaka 2015/16 kwa watu **10,000**. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kwa timu za usimamizi wa uendeshaji wa huduma za afya kwa mikoa ya Dodoma na Ruvuma pamoja na halmashauri zake zote juu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki unaotumika kubaini mahitaji halisi ya watumishi kulingana na uzito wa kazi wa kituo husika (Workload Indicators of Staffing Needs) ili kuweza kufahamu mahitaji halisi ya watumishi katika mikoa hiyo na halmashauri zake.



***20.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka 2015/16, Wizara imeongeza vyuo vinavyoendesha mafunzo kwa njia ya masafa kwa kada ya Tabibu Wasaidizi wanaojiendeleza kuwa Tabibu, kutoka vyuo **3** hadi **8**. Hivyo kufanya ongezeko la wanafunzi wanaochukua mafunzo kwa njia hiyo kufikia **238** kwa mwaka 2015 kutoka **54** kwa mwaka 2012. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya awali juu ya mfumo wa ukusanyaji taarifa za vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii (TIIS) kwa maafisa **4** wa Wizara makao makuu, **24** kutoka vyuo **12** vinavyoendesha mafunzo ya Ustawi wa Jamii nchini.

***21.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17**,** Wizara itafanya maandalizi ya mtaala wa mafunzo ya afya makazini (Occupational Health) na kuendelea na maandalizi ya mtaala wa Radiografia kwa kufuata mfumo wa tuzo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Aidha, Wizara itatoa kipaumbele cha kufadhili mafunzo ya uzamili/uzamivu kwa watumishi ambao maombi yao yatawasilishwa na Taasisi/Hospitali kwa kuzingatia mahitaji kama ilivyoainishwa kwenye ikama (2014-2019). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), itaendesha mafunzo yatakayolenga kuziwezesha Kanda za mafunzo ya Afya, kufuatilia na kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vyote vya Afya nchini.

**_22._** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa afya, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **480** za watumishi wa kada ya afya katika maeneo yaliyo katika mazingira magumu kufikika. Mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilihusu nyumba **310** katika mikoa ya Mtwara, Rukwa/Katavi, Ruvuma, Singida, Pwani, Morogoro, Lindi, Arusha na Manyara. Kati ya nyumba **310**, nyumba **250** zimekamilika na kukabidhiwa kwa halmashauri husika na ujenzi wa nyumba **60** katika mikoa ya Arusha, Manyara na Pwani zipo katika hatua za ukamilishwaji. Awamu ya pili ilihusu nyumba **170** katika mikoa ya Tanga, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Simiyu na Kigoma. Ujenzi wa nyumba hizo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji na unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa kwa halmashauri husika mwezi Juni, 2016.

**_23._** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango wa uimarishaji wa vyuo vya mafunzo ya Sekta ya Afya, Wizara imekarabati na kupanua hospitali na vyuo mbalimbali. Vyuo vilivyofanyiwa ukarabati wa majengo na kukamilika ni Chuo cha Matabibu Lindi na Chuo cha Uuguzi Nzega – Tabora**.** Aidha, ukarabati wa Taasisi ya Afya ya Msingi Iringa na Vyuo



vya Uuguzi vya Songea, Njombe, Rukwa, Mpanda, Kigoma na Ujenzi wa Vyuo vya Uuguzi vya Musoma na Morogoro unaendelea. Ukarabati wa vyuo hivyo unakwenda sambamba na ukarabati wa majengo ya hospitali za rufaa za mikoa husika.

**_24._** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea na upanuzi na ukarabati wa vyuo vya afya vya Mtwara, Tanga, Mirembe na Mvumi. Ujenzi na ukarabati huo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Katika mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha upanuzi na ukarabati wa vyuo hivyo na kuiwezesha Wizara kuongeza idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa.

## HUDUMA ZA KINGA

### Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko

**_25._** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Aidha, utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki umesambazwa na kufikia mikoa **10** ikilinganishwa na mikoa **mitatu** mwaka 2014/15. Vilevile, mafunzo ya utoaji wa

taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yalitolewa kwa jumla ya wataalam **2,315** wa ngazi zote katika Mikoa ya Mwanza (**361**), Geita (**290**), Arusha (**296**), Dodoma (**490**), Singida (**214**), Manyara (**190**), Dar es Salaam – Ilala (**184**) na Kinondoni (**290**). Teknolojia hiyo imerahisisha upatikanaji wa taarifa za magonjwa kwa haraka na hivyo kufanikisha udhibiti wa magonjwa ya milipuko kwa wakati. Utoaji wa taarifa kwa wakati umeongezeka kutoka **asilimia 60** mwaka 2013 hadi **asilimia 75** mwaka 2015.

***26.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia tishio la homa ya Zika lililotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwezi Februari 2016, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa namna ya kudhibiti ugonjwa huo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa ya milipuko ikiwemo Kipindupindu na itapanua utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kwa kuongeza mikoa minne ya Kigoma, Mbeya, Katavi na Rukwa. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua tahadhari ya homa ya bonde la ufa (RVF) kufuatia utabiri wa hali ya hewa unaoonesha kuwa, kutakuwa na mvua kubwa.



***27.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege katika vituo sita maalumu vilivyopo sehemu mbalimbali nchini (sentinel surveillance sites). Vituo hivyo ni pamoja na Hospitali za Mikoa ya Dodoma na Mwanza; Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa ya Hydom (Manyara) na Mwananyamala (Dar es Salaam); Hospitali ya Wilaya ya Kibondo na Kliniki ya 'International School of Tanganyika' ya jijini Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, wastani wa sampuli **3,714** zilichukuliwa na vipimo vya maabara vilionyesha kutokuwepo kwa vimelea vinavyoweza kusababisha mlipuko wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufanya ufuatiliaji katika vituo **6** vilivyopo na inatarajia kuongeza vituo vingine **viwili (2)** katika mikoa ya Mtwara na Kilimanjaro, iliyo mpakani na nchi jirani ili kuweza kutambua ugonjwa huo kwa haraka na kudhibiti uwezekano wa ugonjwa huo kuingia nchini.

### Udhibiti wa Malaria

***28.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kutekeleza afua mbalimbali. Katika mwaka 2015/16,

Wizara ilitekeleza zoezi la kunyunyizia viuatilifu ukoko aina ya *actellic* ndani ya nyumba katika mikoa ya kanda ya ziwa na kufikia nyumba **358,989** ambapo wananchi **1,794,945** walikingwa dhidi ya malaria. Aidha, Wizara imeboresha upatikanaji wa vitendanishi vya kupima malaria na dawa ya mseto kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa malaria isiyo kali katika vituo vyote vya huduma za afya nchini. Jumla ya vitendanishi **17,566,750** vinavyotoa majibu ya haraka (mRDT) na dawa mseto dozi **19,084,230** zilinunuliwa na kutumika katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya. Jumla ya chupa **1,150,000** za dawa ya sindano zilisambazwa kwa ajili ya kutibu wagonjwa wenye malaria kali. Vilevile, uhamasishaji juu ya utekelezaji wa Mkakati wa kuangamiza mazalia ya mbu umefanyika kwa Timu za mikoa na halmashauri saba (7) za Manispaa za Ilemela, Nyamagana, Musoma, Bukoba na Shinyanga, na Miji ya Kibaha na Geita.

***29.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imetekeleza kampeni ya usambazaji wa vyandarua **20,547,849** vyenye viuatilifu vya muda mrefu (LLITNs) katika mikoa **18** ya Mara, Mwanza, Katavi, Tabora, Kigoma, Kagera, Geita, Mbeya, Njombe, Rukwa, Simiyu, Shinyanga, Singida, Iringa, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Vilevile, usajili katika



kaya unaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga, ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ugawaji wa vyandarua.

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na ugawaji wa vyandarua kupitia wanafunzi shuleni na kliniki za afya ya uzazi na mtoto katika mikoa ya Mwanza na Mtwara kwa awamu ya kwanza. Pia, itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi (mRDT) kwa ajili ya kupima uwepo wa vimelea vya malaria na kununua na kusambaza dawa kwa ajili ya matibabu katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za kifua kikuu na kifua kikuu sugu kwa kuboresha huduma za vipimo na kuzisogeza karibu na wananchi. Hivi sasa, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha maabara nne za Kanda za Mbeya (Hospitali ya Rufaa), Mwanza (Bugando), Dodoma (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa) na Kilimanjaro (Hospitali ya Kibong'oto) ambazo zinatarajia kuanza kutoa huduma hivi karibuni. Aidha, Wizara itaendelea na ugatuzi wa matibabu ya kifua kikuu sugu katika

Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Bugando. Vilevile, katika kuimarisha huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI nchini, Wizara imefanikiwa kufikia idadi ya vituo **547** vinavyotoa huduma hiyo chini ya mfumo mmoja. Huduma hiyo inapunguza usumbufu kwa mgonjwa mwenye maambukizi mseto ya Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kupata huduma sehemu moja. Jumla ya Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) **692,642** walipata huduma ya kubainisha uwepo au kutokuwepo kwa maambukizi ya kifua kikuu miongoni mwao. Kati ya waliopata huduma hiyo, **26,218** waligundulika kuwa na maambukizi ya kifua kikuu na walipatiwa matibabu.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya kampeni maalum ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu dalili za ukoma na namna ya kutambua mapema wagonjwa katika hatua za awali za ugonjwa. Kampeni hiyo, imetekelezwa katika wilaya za Kilombero (110), Nanyumbu (30) na Liwale (130) na kusaidia kuibua na kuwaweka katika matibabu jumla ya wagonjwa wapya **270** mwaka 2015.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kugatua huduma za kifua kikuu sugu kufikia hospitali kumi za mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Tanga,



Shinyanga, Geita na Mara. Aidha, Wizara itaiongezea uwezo mikoa 16 yenye viwango vya chini kabisa vya uibuaji wagonjwa wa kifua kikuu ili kuongeza kasi ya kudhibiti ugonjwa huo nchini. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya kampeni maalum za uchunguzi na uibuaji wa wagonjwa wapya wa ukoma katika wilaya zenye viwango vikubwa vya maambukizi zikiwemo wilaya za Liwale, Kilombero, Chato, Nanyumbu, Mkinga na Muheza.

**Udhibiti wa UKIMWI**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti UKIMWI kwa kutoa ushauri nasaha na kupima. Kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2015 jumla ya wateja wapya **3,474,780** walipata ushauri nasaha na kupima VVU. Idadi hiyo inajumuisha pia waliopata huduma kupitia mpango wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU kwa kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Hadi kufikia Desemba, 2015, jumla ya Watu Wanaoishi na VVU (WAVIU) **743,773** walikuwa wameanzishiwa dawa sawa na asilimia **84** ya lengo la kuwafikia WAVIU

**880,681** ifikapo Juni, 2016. Vilevile, Wizara imepanua wigo wa utoaji huduma hizo kwa kuongeza idadi ya vituo zaidi na kufikia vituo **1,677** Desemba, 2015 ikilinganishwa na vituo **1,235** Desemba, 2014.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya tohara kwa wanaume kama mojawapo ya afua ya kupambana na maambukizi ya VVU. Kufikia Desemba, 2015 jumla ya wanaume **444,900** kati ya **492,842** waliolengwa, wamefanyiwa tohara na kufikisha jumla ya wanaume **1,997,000** waliokwisha kupata huduma hiyo tangu ilipozinduliwa nchini mwaka 2010. Idadi hiyo ni sawa na asilimia **71** ya wanaume **2,800,000** wanaopaswa kufikiwa ifikapo mwaka 2017.

***36.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba, vitendanishi na mashine za kupimia wingi wa virusi vya UKIMWI kwenye damu kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa matibabu. Lengo ni kupima **asilimia 50** ya WAVIU wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU ifikapo mwezi Juni, 2017. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watoa huduma **674** kutoka vituo vya kutolea huduma za afya vya mikoa ya Njombe, Dodoma, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Singida, Tabora na Iringa kuhusu kupima



wingi wa virusi vya UKIMWI kwenye damu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutoa huduma ya upimaji VVU na dawa za kupunguza makali ya VVU kwa kuyafikia makundi yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi ya VVU. Vilevile, Wizara itafunga mashine mpya **10** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI katika damu katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dodoma, Tabora, Iringa, St. Francis Ifakara, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Bugando, KCMC, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Maabara ya Taifa ya Viwango na Ubora. Mashine hizo zitasaidiana na mashine **11** zilizofungwa katika hospitali zote za rufaa za kanda. Ongezeko hilo la mashine katika hospitali za rufaa za mikoa litaleta ufanisi katika kutoa vipimo na upatikanaji wa majibu ya vipimo hivyo.

***37.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Afua za Kutokomeza Maambukizi ya VVU toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara iliviboresha vituo vya Mpango wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) kwa kuviwezesha kutoa ARV kwa wajawazito na wanaonyonyesha ili kukinga maambukizi mapya ya VVU kwa watoto na kwa ajili ya kuboresha afya zao. Hadi kufikia Desemba, 2015, kati ya vituo **5,540** vinavyotoa huduma za upimaji wa VVU

na ushauri nasaha, vituo **5,057** vilipata wateja walio na VVU na kuwapa dawa za ARV ili kuzuia maambukizi. Kati ya vituo **5,540**, vituo **4,538** vinatoa huduma ya utambuzi wa mapema wa hali ya maambukizo ya VVU kwa watoto wenye umri wa kati ya wiki 4 hadi 6. Aidha, katika kipindi hicho cha utekelezaji, idadi ya wajawazito na wanawake wanaonyonyesha wanaopata tiba ya ARV imeongezeka kutoka **asilimia 75** mwaka 2013 hadi **asilimia 90** mwaka 2015. Vilevile, watumishi **10,862** walipatiwa mafunzo na stadi husika ili waweze kutoa huduma hizo kwa weledi.

***38.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha Mpango Mkakati wa kutokomeza maambukizi wa VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto (2016-2020). Aidha, Wizara itaendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Vilevile, huduma ya utambuzi wa mapema wa hali ya maambukizo ya VVU kwa watoto wenye umri wa kati ya wiki 4 hadi 6 itaongezeka toka vituo **4,538** vilivyopo hadi **5,068** ifikapo Juni 2017. Pia, Mfumo wa ufuatiliaji wa watoto wanaozaliwa na wanawake wenye VVU ndani ya kipindi cha mwezi mmoja, wanaoandikishwa katika huduma za PMTCT, utasambazwa kutoka mikoa 6 na kufikia mikoa 26 ya Tanzania Bara.



**Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele**

***39.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, ambapo katika mwaka 2015/16, dawa za Kinga-Tiba za magonjwa ya matende na mabusha, usubi, trakoma, kichocho na minyoo ya tumbo ziligawiwa kwa wananchi **28,935,520** walio na umri kati ya miaka **mitano** na kuendelea katika Halmashauri **169** zilizo na viwango vya juu vya maambukizi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na ugawaji wa dawa za kinga tiba katika wilaya zote nchini kulingana na maambukizi ya magonjwa husika. Vilevile, itaendelea na tathmini ya matokeo ya zoezi la kinga tiba mbalimbali ili kufahamu kiwango cha maambukizi husasan ya ugonjwa wa usubi kwa binadamu na wadudu waenezao ugonjwa huo (nzi weusi wadogo) katika wilaya za Muheza, Lushoto, Korogwe, Rungwe na Kyela.

**Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto**

***40.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara imewajengea uwezo watoa huduma

**284** jinsi ya kumhudumia mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu kwa njia ya mwambatano wa ngozi kwa ngozi kati ya mama na mtoto (Kangaroo Mother Care- KMC) katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi. Kufikia Machi, 2016 jumla ya vituo **54** vya KMC vinatoa huduma katika mikoa mbalimbali ya Njombe (**1**), Kigoma (**1**), Mwanza (**1**), Ruvuma (**1**), Kagera (**14**), Pwani (**3**), Dar es Salaam (**2**), Mara (**11**), Lindi (**2**), Mbeya (**4**), Morogoro (**1**), Shinyanga (**1**), Iringa (**1**), Rukwa (**1**), Mtwara (**2**), Tabora (**1**), Tanga (**1**), Kilimanjaro (**2**), Arusha (**1**), Singida (**1**), Dodoma (**1**) na Manyara (**1**).

***41.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma namna ya kumhudumia mtoto mgonjwa mwenye umri chini ya miaka mitano kwa uwiano na kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kutibu Nimonia na kuharisha. Aidha, Wizara itaanzisha vituo **20** vya KMC katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Vilevile, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma wa jinsi ya kumhudumia mtoto mchanga katika vituo vya kutolea huduma vilivyopo katika Kanda ya Ziwa, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini.

***42.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma ya afya kwa watoto chini ya umri wa miaka **mitano**, hususan



kudhibiti magonjwa ya Nimonia na Kuhara, Wizara ilifanya uzinduzi wa matumizi ya dawa ya Amoxycilin myeyuko na Zinki ORS zilizofungashwa pamoja**.** Faida za ufungashaji wa Zinki ORS ni kuboresha upatikanaji, kutolewa kwa pamoja kwa mtoto anayeharisha ili kurudisha maji na chumvichumvi mwilini, kupunguza kiwango cha kuharisha na idadi ya kuharisha kwa siku na kisha kumkinga mtoto na kuharisha kwa kipindi cha miezi 2 au 3. Aidha, Mafunzo elekezi ya matumizi ya dawa hizi mpya yalitolewa kwa Waganga Wakuu, Wafamasia waganga wafawidhi wa hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati katika mikoa na wilaya zote. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya washiriki **2,800** kutoka halmashauri zote **182** walipatiwa mafunzo.

***43.*** ***Mheshimiwa Spika,*** suala la vifo vitokanavyo na uzazi bado limekuwa changamoto. Kutokana na Taarifa ya Umoja wa Mataifa imeeleza kuwa tumeweza kupunguza vifo hivyo kutoka **454** mwaka 2010 hadi vifo **398** mwaka 2015. Ili kuhakikisha vifo hivi vinaendelea kupungua kwa kasi zaidi Wizara imehakikisha, watoa huduma wa afya **2,087** wamejengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya huduma muhimu wakati wa ujauzito, stadi za kuokoa maisha kwa matatizo ya dharura yatokanayo na uzazi na mtoto mchanga, baada ya kujifungua na

huduma muhimu baada ya mimba kuharibika. Aidha, ili kuhakikisha huduma ya afya ya uzazi inakuwa endelevu hadi kuifikia jamii, wahudumu wa afya ngazi ya jamii **917** walipatiwa mafunzo jumuishi ya afya ya uzazi na mtoto. Vilevile, jamii imeendelea kuelimishwa kupitia luninga na redio kwa programu ya "Wazazi Nipendeni", kupitia simu ya kiganjani ambapo wanawake wajawazito hujisajili kwa namba 15001 na kuweka neno "mimba" ili kupata taarifa ya huduma anazostahili kupatiwa kulingana na umri wa mimba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Pia, jamii inaweza kujisajili kwa namba hiyohiyo na kuweka neno "mtoto" ili kupatiwa elimu ya masuala ya uzazi. Aidha, vituo vya afya vimeendelea kuboreshwa na kupandishwa ngazi kwa kuanza kufanya upasuaji wa kutoa mtoto kutokana na uzazi pingamizi. Hadi sasa viko vituo **159** vinavyotoa huduma hizo. Vilevile, jamii imeendelewa kuhamasishwa kuhusu kujitolea kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wanawake kwa matatizo yatokanayo na uzazi. Aidha, Halmashauri zimeendelea kuhamasishwa kuhakikisha magari ya kubebea wagonjwa yanapatikana katika vituo vya kutolea huduma ili kutoa rufaa mapema endapo itahitajika katika kuokoa maisha



**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kutoa huduma za dharura kwa wanawake wajawazito, kuhimiza Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye uzazi salama na kushirikisha wananchi na jamii kwa ujumla juu ya kutokomeza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Sote tuwajibike, tuweke nguvu kwa pamoja tutaweza kushinda vita hii na kuwahakikishia wanawake usalama wao na wa watoto wao wanapotekeleza haki yao ya msingi ya uzazi. Wizara itaanza kutoa taarifa kila baada ya robo mwaka ya vifo vitokanavyo na uzazi vilivyotokea katika kila Halmashauri ili kuongeza uwajibikaji katika Halmashauri na jamii husika. Tuwajibike kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Aidha, Wizara inaipongeza Serikali ya kijiji cha Utulo, Halmashauri ya Mbarali kwa kuweka mkakati wa kudhibiti vifo katika jamii yao ambapo toka mwaka 1998 hakuna vifo vya uzazi vilivyoripotiwa katika zahanati ya kijiji cha Uturo

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, Wizara pia imeendelea kuimarisha huduma za uzazi wa mpango kwa kusambaza dawa na vifaa pamoja na kuwajengea uwezo watoa huduma. Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara imenunua kondomu za kiume **9,000,000**; Dawa ya sindano (Depo provera)

vichupa **2,908,043**; Vipandikizi (Implants) **1,313,004**; Vitanzi (IUDs) **211,500** na Dawa za vidonge mizunguko (cycles) **544,320.** Aidha, watoa huduma **989** wamejengewa uwezo ikilinganishwa na lengo la watoa huduma **780** ili waweze kutoa huduma za uzazi wa mpango kwa ufanisi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango. Aidha, tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati wa huduma za uzazi wa mpango uliothaminiwa kwa kipindi cha miaka mitano (2010-2015) itafanyika. Matokeo ya tathmini hiyo yatatoa mwelekeo wa mambo muhimu yatakayotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2016-2021.

***46.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wengine kukabiliana na kuhudumia wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa kuwapatia mafunzo watoa huduma. Hadi Machi, 2016, jumla ya watoa huduma **316** wamejengewa uwezo. Vilevile, jumla ya wahanga **42,390** ambao wanawake ni **32,103** sawa na **asilimia 76** na watoto wenye umri chini ya miaka 18 ni **3,985** sawa na **asilimia 9.4** walipatiwa huduma za matibabu na uchunguzi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaongeza vituo vya kutoa huduma toshelezi katika mikoa ya Simiyu (Maswa), Shinyanga (Kahama) na Pwani (Kibaha). Vilevile,



Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa, kuboresha mfumo wa rufaa na ukusanyaji wa ushahidi wa kimahakama kwa waliofanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Kufikia Machi, 2016, vimeanzishwa vituo vipya **12** vya uchunguzi na matibabu katika mikoa ya Arusha, Shinyanga, Lindi, Morogoro na Mwanza hivyo kufanya jumla ya vituo **298** vilivyopo katika Mikoa 26 ya Tanzania bara (**Kiambatisho Na. 1**). Jumla ya wanawake **120,011** walipimwa ambapo **2,060** waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na walipatiwa matibabu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi.

**Huduma za Chanjo**

***48.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za Chanjo kulingana na Sera na Miongozo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa chanjo,

imehakikisha kuwepo kwa chanjo za kutosha kwa ajili ya huduma za chanjo nchini kwa watoto na makundi mengine kwa kununua na kusambaza chanjo katika mikoa na halmashauri zote nchini. Mnamo Novemba, 2015 Tanzania ilipata cheti cha kuwa mojawapo ya nchi isiyokuwa na virusi vya ugonjwa wa polio. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa chanjo ya polio ili kuendelea kuhakikisha uwepo wa kinga dhidi ya virusi vya polio katika jamii. Vilevile, Wizara ilinunua magari **58** ambayo yaligawanywa katika halmashauri zilizokuwa na uhaba mkubwa wa magari zikiwemo halmashauri mpya. Pia, pikipiki **40** ziligawanywa katika baadhi ya Halmashauri ili kuboresha ufuatiliaji wa magonjwa kwa lengo la kudhibiti milipuko ya magonjwa yanayokingwa kwa chanjo.

***49.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilinunua na kusambaza baiskeli **968** katika halmashauri zote kwa ajili ya kuimarisha huduma za mkoba katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa chanjo, ili kuwafikia watoto wote na kuwapatia chanjo **(Kiambatisho Na. 2)**. Aidha, vituo **37** vya mikoa ya Geita, Njombe, Tabora, Iringa, Mwanza, Arusha, Dodoma, Lindi na Manyara vilifungiwa majokofu ya umeme-jua sambamba na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa majokofu hayo, utunzaji wa chanjo na vifaa vya



kutolea chanjo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuongeza kiwango cha chanjo hadi kufikia **asilimia 95** na kuongeza kiwango cha utunzaji chanjo kwa kununua majokofu ya kutunzia chanjo hadi **asilimia 90** ya mahitaji kwenye ngazi ya Halmashauri.

**Usafi wa Mazingira**

***50.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira kwa lengo la kuhimiza jamii kujenga na kutumia vyoo bora. Kufuatia uhamasishaji huo, jumla ya kaya **479,011** kati ya kaya **554,000** sawa na asilimia **86.4** ya lengo zimejenga vyoo bora. Idadi hiyo inafanya jumla ya vyoo vyote vilivyojengwa tangu kuanza kwa utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira mwaka 2013 kufikia **1,030,817**. Vyoo bora vilivyojengwa mashuleni ni **1,630** na kuvuka lengo la vyoo **812**.

***51.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendesha zoezi la usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira ili kuimarisha utekelezaji wa afya katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Katika mwaka 2015/16, zoezi la ufuatiliaji wa Kampeni hiyo lilitekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya

kwanza Mikoa 15 ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Shinyanga, Geita, Simiyu na Halmashauri zote katika mikoa hiyo ilitembelewa. Awamu ya pili ilihusisha Mikoa mingine iliyobakia ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Mwanza, Kagera na Mara. Aidha, Wizara imeanza hatua za manunuzi ya pikipiki **100** ili kuimarisha ufuatiliaji ngazi ya halmashauri. Vilevile, utekelezaji wa Mfumo wa uhifadhi taarifa za usafi wa mazingira wa kielektroniki umeshaanza kutumika katika mikoa 13 ya majaribio ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Iringa, Njombe, Mbeya, Mwanza, Kagera, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Mara na Tabora. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira katika mikoa na halmashauri zote nchini. Ni wajibu wa kila halmashauri kuweka mikakati madhubuti ya usafi wa mazingira katika maeneo yake. Wizara inapongeza jitihada za Mheshimiwa Rais, wa awamu ya tano kwa kuweka msisitizo katika usafi wa mazingira. Aidha Wizara inatambua kazi nzuri ya **Mheshimiwa Paul Makonda** Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam kwa kuzindua kampeni ya usafi katika mkoa wa Dar es Salaam.



***52.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara iliwahamasisha viongozi wa ngazi ya Mkoa kwa Mikoa ya Kigoma na Dodoma na Halmashauri za Manispaa ya Kigoma na Wilaya ya Kongwa juu ya athari za kiafya zitokanazo na mabadiliko ya Tabia nchi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendesha mafunzo kwa Watendaji wa Mamlaka ya Maji safi na maji taka Manispaa ya Kigoma na Kikundi cha watumia maji cha Mbande kilichopo katika Wilaya ya Kongwa. Mafunzo hayo yatajenga uwezo wa mamlaka hizo ili ziweze kuchukua hatua stahiki zitakazowezesha upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yao kutokana na athari zinazoweza kutokea na mabadiliko ya mara kwa mara ya Tabia nchi.

***53.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuvijengea uwezo vituo vyake vya mipakani **10** kwa madhumuni ya kujikinga na magonjwa yanayotolewa taarifa kimataifa na athari nyingine za kiafya pamoja na kudhibiti wasafiri kuwa na chanjo ya homa ya manjano pale inapotakiwa. Aidha, katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha udhibiti wa magonjwa mipakani kwa kuhakikisha kuwa chanjo ya homa ya manjano inasimamiwa na pale msafiri anapokutwa hajachanja ipasavyo atachanjwa na siyo kugongewa kitabu. Wizara itaweka adhabu kali kwa wote watoa huduma na wasafiri ambao watakiuka utaratibu huu.

### Elimu ya Afya kwa Umma

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa na kufanya uchunguzi wa afya ikiwemo saratani ya tezi dume. Aidha, Wizara ilitayarisha na kusambaza vielelezo vya kuelimisha jamii kuhusu saratani ya tezi dume (vipeperushi **100,000**) na ugonjwa wa kipindupindu (mabango **267,000**; bango kitita **7,000;** vipeperushi **640,000;** DVDs **7000;** CDs **2,000)**. Vilevile, kutokana na ugonjwa wa kipindupindu kuathiri takriban nchi nzima, Wizara ilitumia njia za ziada ili kuifikia sehemu kubwa ya jamii zikiwemo mitandao ya kijamii, matangazo kwa njia ya radio (**29**) na televisheni (**7**); huduma za simu bila malipo kupitia nambari 17554 kwa kutuma neno kipindupindu au kupiga simu nambari 117 kuelimishwa au kuongea na mtaalamu. Pia, wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao **1,070** walijengewa uwezo wa kuhamasisha jamii nyumba hadi nyumba kwa kutumia bango kitita. Wizara ilihakiki vielelezo mbalimbali vilivyotayarishwa na wadau ili kuona iwapo vina ubora unaotakiwa na iwapo vimezingatia Sera na Miongozo ya Wizara. Vielelezo hivyo ni pamoja na vile vya uzazi wa mpango, afya ya uzazi, mama na mtoto, lishe, chanjo,



UKIMWI, kifua kikuu, afya ya mazingira, magonjwa yanayoambukiza na yasiyo ya kuambukiza, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, malaria, afya ya kinywa na macho.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya kupitia njia zote za mawasiliano ili kuifikia jamii, ikiwemo machapisho, vyombo vya habari, simu za mkononi, njia za asili, mitandao ya kijamii na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kufanya uhamashishaji wa nyumba hadi nyumba.

### Huduma za Lishe

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2015/16, Serikali imevuka lengo la kuhamasisha viwanda vinavyosindika vyakula ili kuongeza virutubishi aina ya vitamini na madini kufikia 21 ikilinganishwa na viwanda 13 mwaka 2014/15. Viwanda vilivyoongezeka ni *Basic Elements Ltd* (DSM), *Sunkist Group Ltd* (Arusha), Mount Meru (Arusha), VOIL Mwanza (Mwanza), *GM Medol* (DSM) pamoja na viwanda vitatu vya kati vya kusindika mafuta na kuongeza vitamini A vilivyopo Babati na Singida. Serikali pia imeanza kupanua wigo

wa kuongeza virutubishi kupitia vinu vya kusagisha unga wa mahindi ngazi ya vijiji, ambapo jumla ya vinu **290** katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Morogoro, Dodoma na Arusha vinasaga mahindi na kuongeza virutubishi vya madini na vitamini.

***57.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Wizara imenunua tani **93** za virutubishi (Premix) katika mwezi Agosti na mwezi Novemba, 2015. Virutubishi hivyo vilisambazwa kupitia Bohari ya Dawa kwenda wilaya sita zenye mradi wa majaribio wa kuongeza virutubishi katika unga wa mahindi zilizopo Mikoa ya Njombe (Njombe Mji), Iringa (Iringa Vijijini na Kilolo) na Arusha (Meru, Monduli na Karatu). Vilevile, **katoni 805** zenye jumla ya vipaketi **milioni 4.8** zilinunuliwa kwa ajili ya watoto walio na umri chini ya miaka mitano na tayari pakiti **milioni 1.52** zimesambazwa **(Kiambatisho Na. 3)**. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kushirikiana na asasi zisizo za serikali kuhakikisha virutubishi muhimu kwa ukuaji na ufanisi wa mwili vinaendelea kupatikana na kufikia wilaya nyingine nchini.



## HUDUMA ZA TIBA

### Huduma za Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda

***58.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Taifa Muhimbili** imehudumia jumla ya wagonjwa **299,769**. Kati yao, **256,888** walikuwa wagonjwa wa nje na **42,881** ni wagonjwa waliolazwa. Vilevile, katika kutekeleza mkakati wa Serikali wa kupambana na tezi dume, hospitali iliwafanyia uchunguzi jumla ya wagonjwa **4,054**. Wagonjwa wa nje waliopatiwa tiba ya upasuaji walikuwa **6,021**, mishipa ya fahamu walikuwa **3,855** na waliopatiwa matibabu ya figo walikuwa **10,040,** ikiwemo mizunguko **6,292** ya kusafisha figo. Vitanda vya kulaza wagonjwa vimeongezeka kutoka **1,354** mwaka 2014/15 hadi **1,643** mwaka 2015/16. Aidha, katika mwaka 2016/17, hospitali itaongeza idadi ya vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) kutoka vitanda **21** vya sasa hadi vitanda **75**, itanunua vifaa tiba vya upasuaji na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka **13** vya sasa hadi **18**, itapanua huduma za kusafisha figo kwa kuongeza vitanda kutoka vitanda **15** vya sasa hadi vitanda **50** na kuanza kusafisha figo kwa watu wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI na virusi vya ini. Aidha, hospitali itaanzisha huduma mpya za upandikizaji wa figo (*renal transplant*) na

upandikizaji wa "*cochlea*" kwa wagonjwa ambao ni viziwi. Vilevile, hospitali itaboresha huduma za kulaza wagonjwa binafsi na kujenga jengo la kisasa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa binafsi na viongozi wa kitaifa na watu mashuhuri litakalokuwa na jumla ya vitanda **170** na kuongeza mapato ya ndani kutoka shilingi **bilioni 2.6** za sasa hadi shilingi **bilioni tano** kwa mwezi.

***59.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Wizara imeanzisha **Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete**. Aidha, Taasisi hiyo iliwahudumia wagonjwa **24,570** wa nje na wagonjwa **2,134** waliolazwa. Jumla ya wagonjwa **207** walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo ambapo kati yao, watoto chini ya umri wa miaka 18 walikuwa **178**. Kwa kufanya upasuaji huo hapa nchini, Taasisi imeweza kuhudumia wagonjwa wengi zaidi kuliko ambavyo huduma hii ingepatikana nje ya nchi na kuokoa zaidi ya **shilingi bilioni nne** za Serikali. Vilevile, Taasisi imeanza kupokea wagonjwa kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Nigeria na Comoro.

***60.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilifanya uchunguzi kwa wagonjwa wa magonjwa ya moyo **451** kwa kutumia mashine ya kisasa (Cath Lab.). Mashine hiyo



inamuwezesha daktari kuweka vyuma maalum ndani ya mishipa ya moyo "stents", mashine za kuendesha moyo (pacemarkers) na kuziba matundu bila kupasua kifua. Kati ya wagonjwa **451** waliotibiwa, ni kifo kimoja tu kilitokea. Aidha, Taasisi iliongeza uwezo na uzoefu kwa wataalam wake kupitia kambi zilizohusisha wataalam toka taasisi za nje ya nchi zenye uzoefu wa miaka mingi zaidi katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa moyo na mishipa ya damu. Katika mwaka 2016/17, Taasisi itaendelea kuboresha huduma na kuifanya kuwa kituo cha mafunzo kwa wataalam wa upasuaji wa moyo Afrika Mashariki na Kati. Aidha, Taasisi itaongeza idadi ya kambi za upasuaji wa kibingwa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nje ya nchi. Hii itatoa fursa kwa wataalam wa Taasisi kujifunza zaidi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaijengea uwezo Taasisi kwa kuweka vifaa ili chumba cha upasuaji cha 3 kianze kufanya kazi.

***61.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Serikali imeanzisha **Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa** iliyopo Chuo Kikuu cha Dodoma. Kuanzia Oktoba, 2015 hadi Machi, 2016, Hospitali hiyo iliyopewa hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati imehudumia wagonjwa **6,450**. Kati yao, **1,747** ni wagonjwa waliolazwa na **4,520** ni wagonjwa wa nje. Aidha,

wagonjwa **183** waliopata huduma ya upasuaji na wanawake **102** waliojifungua.

*62.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, **Taasisi ya Mifupa Muhimbili** (MOI) imehudumia Wagonjwa **81,106**. Kati yao wagonjwa **74,711** walikuwa wagonjwa wa nje na **6,395** wagonjwa wa kulazwa. Aidha, Taasisi ilifanya upasuaji mkubwa kwa wagonjwa katika maeneo yafuatayo; ubongo (**278)**, uti wa mgongo (**101)**, nyonga (**278)**, goti (**25)**, mifupa mikubwa (**5,827), vichwa vikubwa kwa watoto (**855)** na pia kuwawekea viungo bandia wahitaji. Taasisi imeweza kushinda tuzo ya mwaka ya utafiti bora Duniani kuhusu upasuaji wa mfupa wa paja kwa mwaka 2015 inayotolewa na Orthopaedic and Trauma Association (OTA) ya San Diego, Marekani.

*63.* ***Mheshimiwa Spika*, **katika mwaka 2016/17, Taasisi ya MOI itaongeza nafasi ya wagonjwa wanaolazwa kutoka vitanda **150** hadi **340** ambapo katika chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) vitaongezeka kutoka vitanda **8** hadi **32**. Katika kuijengea uwezo Taasisi, Serikali itanunua mashine mpya za uchunguzi ikiwa ni pamoja na MRI, CT Scan na Digital Xrays. Aidha, Taasisi itatoa mafunzo na upasuaji wa marejeo kwa nyonga na goti. Vilevile, mfumo mpya wa kieletroniki utafungwa ili kuboresha huduma na makusanyo



ya maduhuri. Pia, huduma za kibingwa za mkoba (outreach services) zitatolewa katika hospitali za Temeke, Amana - Ilala, Mwananyamala - Kinondoni, Tumbi - Kibaha na Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Morogoro.

*64.* ***Mheshimiwa Spika*, Taasisi ya Saratani Ocean Road** ilihudumia jumla ya wagonjwa **31,075**, kati yao wagonjwa wa saratani walikuwa **17,819** na wagonjwa wa kawaida ni **13,256**. Taasisi iliwafanyia uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti wanawake **5,367**, kati yao **435** waligundulika kuwa na dalili za awali za saratani ya mlango wa kizazi na **149** waligundulika kuwa na dalili za awali za saratani ya matiti.

*65.* ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Saratani kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi kwa wanafunzi **27** na Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani kwa wataalamu **13** kwa lengo la kuongeza wataalamu wa kuchunguza, kupima na kutibu saratani nchini. Aidha, Taasisi iliendelea na ujenzi wa "bunkers" kwa ajili ya kuweka mashine mpya za kisasa za kutibu saratani. Utaratibu wa kununua mashine moja ya LINAC unaendelea. Lengo

ni kupunguza mrundikano wa wagonjwa wanaosubiri kwa kipindi cha muda mrefu kupata matibabu ya mionzi.

***66.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha huduma za kinga na uchunguzi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, kwa kuipatia vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na PET/CT Scan, *LINAC* na MRI. Aidha, Taasisi itaimarisha huduma za mkoba hasa katika maeneo ambayo yanaonekana kuwa na idadi kubwa ya watu waliogundulika kuwa na saratani. Vilevile, Wizara itaimarisha upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani ambapo asilimia 13 ya fedha za dawa itatumika kununua dawa za saratani ili kupunguza mzigo kwa wagonjwa hasa wa kipato cha chini.

***67.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Mirembe** ilihudumia jumla ya wagonjwa **33,900**, kati yao wagonjwa wa akili **1,926** walilazwa na wengine **31,772** walihudumiwa na kurudi nyumbani. Aidha, wagonjwa wa akili wahalifu wapya **211** walipokelewa na kuhudumiwa kwa mujibu wa sheria katika Taasisi ya Isanga. Vilevile, watumishi wapatao **55** walipatiwa mafunzo ya huduma ya tiba kwa waathirika wa madawa ya kulevya ili waweze kuboresha huduma kwa wagonjwa hao.



***68.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa na Hospitali ya Mirembe. Itakarabati miundombinu ya kutolea huduma pamoja na kuweka mfumo wa kielectroniki wa Hospitali kwa awamu ya pili wa WEBERP. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa watumishi ili kukidhi mahitaji ya kutoa huduma kwa waathirika wa madawa ya kulevya.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika***, **Hospitali ya Kibong'oto** ilihudumia jumla ya wagonjwa wa nje **22,348** na wagonjwa **575** wa kifua kikuu walilazwa. Kati ya waliolazwa, waliokuwa na Kifua Kikuu Sugu walikuwa **114** na wagonjwa wa UKIMWI **130**. Aidha, hospitali iliendelea kutoa huduma za usimamizi shirikishi kwa wagonjwa **140** wa Kifua Kikuu Sugu kwa vikoba kutoka katika Mikoa 18. Vilevile, Hospitali ilitoa mafunzo ya kuwahudumia Wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu kwa wataalamu **50** wanaotoka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, na Hospitali za Rufaa Mbeya na Bugando. Katika mwaka 2016/17, Hospitali ya Kibong'oto itaboresha mifumo ya uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko kwa Kanda ya Kaskazini pamoja na kutoa huduma za mikoba za Kibingwa kwa hospitali zinazotoa huduma za Kifua Kikuu Sugu.

70. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Bugando** imehudumia jumla ya wagonjwa **327,080**. Idadi hiyo ilijumuisha wagonjwa wa nje **291,840** wagonjwa wa ndani **35,240**. Aidha, jumla ya wagonjwa **7,536** walifanyiwa upasuaji na kati yao wagonjwa **88** walifanyiwa upasuaji wa moyo na kifua, ambapo wagonjwa **12** walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo. Jumla ya wagonjwa **3,392** walipata matibabu ya saratani. Vilevile, Hospitali imefanya upasuaji kwa Wanawake **148** wenye matatizo ya fistula (*VVF)* na imefanikiwa kununua mashine nyingine ya *Varian LINAC* ya matibabu ya ugonjwa wa saratani na kufanya mashine za *LINAC* kuwa **2**. Pia, Hospitali imefunga CCTV Cameras **185** kuimairisha ulinzi na usalama na kununua mashine kubwa ya kufua hewa ya Oksijeni na tayari mabomba yamefungwa kusambaza hewa hiyo kwenye wodi zote **12** zinazohitaji uangalizi wa karibu.

71. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, **Hospitali ya Bugando** itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwa pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la saratani, na kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Aidha, Hospitali itafunga mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za hospitali. Vilevile,



Hospitali itafunga CT-Scan simulator kwa ajili ya kupanga matibabu na mashine mbili za *VARIAN & ELEKTA LINAC* kwa ajili ya matibabu ya saratani. Hatua hiyo itasaidia wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa kupata huduma ya matibabu ya mionzi Mwanza badala ya Dar es Salaam.

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Rufaa ya KCMC** ilihudumia jumla ya wagonjwa **223,198**. Kati yao wagonjwa wa nje ni **198,799** na wagonjwa wa kulazwa ni **24,399**. Baadhi ya huduma zilizotolewa kwa wagonjwa hao ni pamoja na macho **2,273**, upasuaji kwa njia ya tundu dogo **102**, upasuaji katika mfumo wa mkojo **141** na aina mbalimbali za upasuaji **406**. Aidha, Hospitali ilifanya vipimo vya viashiria vya saratani ya mlango wa kizazi pamoja na matiti kwa wanawake **1,095** ambapo wanawake **29** waligundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi na walipewa matibabu pamoja na Rufaa kwenda Hospitali ya Ocean Road kwa matibabu zaidi. Vilevile, ujenzi wa jengo la huduma za dharura umekamilika.

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Hospitali ya Rufaa KCMC itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za saratani, Kitengo cha moyo na kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Aidha, Hospitali itaendelea kutoa huduma

za magonjwa ya ngozi na kufungua wodi mpya za wagonjwa walioungua kwa moto na kemikali. Vilevile, itaanzisha kitengo cha ICU kwa ajili ya watoto na itanunua vifaa vya uchunguzi wa magonjwa vya CT Scan, MRI pamoja na vifaa kwa ajili ya jengo jipya la huduma za dharura.

***74.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Rufaa ya Kanda – Mbeya** ilinunua na kufunga mitambo ya upasuaji kwa kutumia tundu dogo na kutoa mafunzo kwa wataalam watakaokuwa wakitumia mitambo hiyo. Aidha, jumla ya wagonjwa **32** ambao figo zao hazifanyi kazi ipasavyo walihudumiwa kwa damu zao kuchujwa, ambapo zaidi ya mizunguko **1,022** ilifanyika.

***75.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17, Hospitali itaanzisha huduma za upasuaji maalum kwa kutumia tundu dogo. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili itaboresha huduma za upasuaji kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa fahamu. Vilevile, Hospitali itaboresha huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo kwa kuwawekea *Arterial Veinosis Fistula* wagonjwa wa figo wanaochujwa damu badala ya kutumia njia inayotumika sasa ya *Temporal Catheter*.



***Usimamizi wa utoaji wa Huduma za Tiba Nchini***

***76.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, katika kuhakikisha Wizara inafanyia kazi kwa wakati na kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu ubora wa huduma, Wizara imetoa maelekezo kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini kuweka utaratibu mwepesi kwa wananchi kufikisha malalamiko yao pindi wanapoona kwamba hawakupatiwa huduma za afya kwa kiwango stahiki. Utaratibu huu unajumuisha uwekaji wa namba za simu za viongozi wa afya wa mkoa, halmashauri pamoja na wasimamizi wa vituo vyote vya kutolea huduma vya umma. Katika mwaka 2016/17 Wizara itaendeleo kuhakikisha vituo vyote vya umma vinaweka namba zao viongozi husika katika eneo la wazi na rahisi kuonekana ili kuwezesha wananchi kutoa malalamiko yao na kupata ufumbuzi mara moja.

***77.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile katika mwaka 2016/17 Wizara itaendeleo kupokea malalamiko na kero za wananchi kupitia kituo cha kushughulikia malalamiko kwa huduma za Bima ya afya. Huduma hii ya simu kuanzia sasa itatumika na wananchi wote hata wasio wa wanachama wa Bima ili kutoa kero zao pale ambapo hazikutatuliwa katika ngazi za chini. Simu hiyo

ni bure na namba yake ni **08001163**. Aidha, namba hizi zitabandikwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma nchini. Vilevile, Wizara itaimarisha usimamizi wa huduma za tiba Kikanda kwa kuanzisha Madawati maalum ambayo yatasimamiwa na Maafisa Maalum ili kuhakikisha utoaji huduma unasimamiwa kwa karibu na malalamiko yote yanafanyiwa kazi haraka. Madawati haya yatagawanywa katika Kanda **9** ambazo ni Maalum (Dar Es Salaam), Kusini (Mtwara na Lindi), Mashariki (Pwani na Morogoro), Magharibi (Kigoma na Tabora), Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Njombe na Songea), Nyanda za Juu Kusini Magharibi (Mbeya, Songwe, Katavi na Rukwa), Ziwa (Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara na Mwanza), Kaskazini (Tanga, Manyara, Arusha na Kilimanjaro), Kati (Singida na Dodoma).

***78.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Katikka mwaka 2015/16 uongozi wa juu wa Wizara tumekuwa umetembelea vituo vya kutolea huduma za afya kwa lengo kufuatilia utuaji wa huduma kwa wananchi na pia kusikia kero zao. Hadi ya Aprili 2016, hospitali za Rufaa Mikoa yote nchini na baadhi ya hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati vimetembeleo. Tumeona mambo mazuri yanayotekelezwa na watoa huduma wetu lakini pia tumeona changamoto kubwa inayoikabili sekta ya



afya ikiwemo dawa, upungufu wa watumishi na huduma zisizo kidhi ubora wa huduma.

***Huduma za Matibabu kwa Wazee***

***79.*** ***Mheshimiwa Spika*****;** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu utolewaji wa huduma ya matibabu bure kwa wazee. Katika kutekeleza azma hiyo, vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika halmashauri, mikoa na rufaa vimeelekezwa kutenga dirisha maalum kwa ajili ya matibabu ya wazee. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya madirisha ya wazee **24** katika hospitali za mikoa na **133** katika hospitali za halmashauri yametengwa kwa ajili ya matibabu ya wazee. Aidha, mwezi Aprili, 2016, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilizindua Kampeni ya **Mzee Kwanza,** ili kuhamasisha Jamii kutoa umuhimu na kipaumbele kwa Wazee katika huduma ikiwemo huduma za matibabu. **Kampeni** inasisitiza watoa huduma na wananchi kutoa kipaumbele kwa wazee katika kupata huduma za afya.

***80.*** ***Mheshimiwa Spika*****;** Wazee ni hazina, hivyo Wizara inaelekeza uongozi wa vituo vya afya vya umma siyo tu kutenga dirisha la wazee bali kuweka sehemu maalum

ya kutolea huduma kwa wazee ili kuwapunguzia usumbufu Waganga Wafawidhi wanawajibu wa kuhakikisha kuwa wazee wanapata dawa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuhamasisha halmashauri kuweka utaratibu wa kuwakatia Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma ya afya kwa kundi hilo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaandaa mkakati wa kuboresha huduma za afya kwa wazee, itaboresha upatikanaji wa takwimu zinazohusu wazee katika ngazi zote za kutolea huduma, itahakikisha kuwa dawa zinazotakiwa kutibu magonjwa yanayowasibu wazee mara kwa mara zinapatikana kwa kutenga fedha maalum kwa ajili ya kununulia dawa hizo na itaboresha sehemu inayoratibu huduma za afya kwa wazee katika ngazi zote

**Huduma za uchunguzi**

***81.*** ***Mheshimiwa Spika*** katika 2015/16, Jumla ya maabara **18** ziliingizwa katika mchakato wa kuinua viwango vya ubora wa huduma za maabara kwa utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa nyota za ithbati hatua kwa hatua na kufikia jumla ya maabara **66**. Kati ya hizo, maabara **25**, zimefikia viwango vya ubora wa nyota 1 hadi 3. Aidha, Wizara iliendelea kusimamia



utoaji wa ithbati kwa viwango vya kimataifa (ISO 15189) kwa Maabara za ngazi ya Taifa na Kanda. Maabara ya KCMC ilipewa ithibati mwezi Julai, 2015 na kufanya jumla ya maabara za Afya zenye ithibati ya kimataifa kuwa tano (5); ambazo ni Maabara ya Taifa ya Ubora na Mafunzo (NHLQATC), Bugando, Mbeya Rufaa na Muhimbili.

***82.*** ***Mheshimiwa Spika*** katika 2016/17**,** Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha viwango vya ubora wa huduma za maabara ngazi ya mikoa, wilaya na Vituo vya Afya, kwa utaratibu wa Shirika la Afya Duniani, wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, kwa kutoa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia na kuimarisha huduma za Maabara za Afya za Jamii kwa kuifanya Maabara ya Taifa ya Afya za Jamii kutambuliwa kisheria na kuwa Taasisi inayojitegemea kwa kuanza ujenzi wa maabara hiyo katika eneo la Mabibo, Dar es salaam.

***83.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za uchunguzi kwa kufanyia matengenezo na kununua vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika mwaka 2015/16, mashine mpya za kisasa za radiolojia za *CT scan*, *Digital X-Ray* na *Ultrasound* zimefungwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Aidha, Mafunzo ya

matengenezo na matumizi ya vifaa tiba yalitolewa kwa watalaam **30** wa ufundi wa vifaa tiba toka katika hospitali za Halmashauri, Mikoa na Karakana za Kanda ili kuwaandaa kuweza kufanya matengenezo ya vifaa katika maeneo yao.

***84.*** ***Mheshimiwa Spika*** katika 2016/17**,** Wizara itaboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya mionzi kwa kutekeleza Mradi mpya wa ORIO. Mradi huo utaboresha huduma za radiolojia kwenye jumla ya hospitali **37** ambapo kati ya hizo hospitali **7** ni za Wilaya, **23** za Rufaa za Mikoa na **7** za Kanda na Taifa. Mradi huo utahusisha uboreshaji wa huduma za uchunguzi wa radiolojia kwa wagonjwa, wanawake wajawazito, na watoto chini ya miaka 5 katika hospitali husika. Aidha, Wizara itatoa vifaa tiba, itakarabati majengo na miundo mbinu, itatoa mafunzo maalum kwa watumiaji na wahandisi/mafundi wa vifaa tiba na pia mpango wa matengenezo kinga ambao utatekelezwa kwa miaka 5. Kwa kuwa sehemu kubwa ya tiba ni uchunguzi, Wizara inazielekeza halmashauri kuweka kipaumbele katika kuboresha huduma za uchunguzi kwa kununua vifaa ikiwemo x-ray, ultrasound kwa ajili ya hospitali za wilaya na vituo vya afya.



**Huduma za Damu Salama**

***85.*** ***Mheshimiwa Spika*** katika 2015/16, Wizara iliendelea kusimamia na kuimarisha huduma za Damu Salama. Jumla ya chupa **71,600** kati ya chupa **140,000** zilizokusudiwa kwa mwaka sawa na asilimia **51** zilikusanywa. Aidha, Wizara, imewajengea uwezo watumishi watatu katika kila Halmashauri za mikoa 12 ya Kagera, Simiyu, Mara, Kigoma, Pwani, Mbeya, Dar es Salama, Manyara, Lindi, Arusha, Katavi na Rukwa ili waweze kukusanya damu. Katika 2016/17, Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo vya kukusanya damu salama katika mikoa ya Iringa, Simiyu, Mara, Geita na Mwanza. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha halmashauri zote kusimamia zoezi la ukusanyaji na uhifadhi wa damu. Ninatoa rai kwa wananchi kuchangia damu.

**Huduma za kinywa**

***86.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara ilitengeneza vipeperushi na mabango ya kufundishia elimu ya afya ya kinywa mashuleni na kutoa elimu hiyo katika shule za msingi zilizopo katika majiji ya Mwanza (Nyamagana), Tanga na Mbeya. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza mashine nne (4) za

kutibia meno ambazo zimefungwa katika hospitali tatu (3) za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dar es salaam (Amana) na Kagera, na pia hospitali ya Mgulani JKT. Vilevile, Wizara ilifanya matengenezo ya vifaa na mashine za kutibia meno katika kliniki za meno zilizopo katika hospitali za rufaa za mikoa ya Dodoma, Mtwara, Dar es salaam (Amana na Temeke), Iringa, hospitali ya Mbagala Rangi Tatu (Dar es salaam) na Chuo cha Tabibu Meno Tanga.

***87.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma za tiba ya kinywa na meno, katika mwaka 2016/17, Wizara itanunua jumla ya mashine nne (4) za kutibia meno na kuzisambaza katika hospitali za rufaa za mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Tanga, na Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Aidha, Wizara itafanya matengenezo kinga ya vifaa na mashine za kutibia meno katika kliniki za meno za mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Tanga. Vilevile, katika kuboresha huduma za kinga kwa magonjwa ya kinywa na meno, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wake wa kuboresha elimu ya afya ya kinywa na meno mashuleni katika majiji ya Mbeya, Mwanza na Tanga. Mpango huo umelenga kuongeza uelewa kwa watoto wa shule juu ya kujikinga na magonjwa ya kinywa na meno.



**Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

***88.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Dawa za Asili Muhimbili – MUHAS ilitoa mafunzo kwa waganga wa tiba asili na tiba mbadala **25** kuhusu namna bora ya kutengeneza dawa za asili. Aidha, wanafunzi **59** wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa walipata mafunzo kuhusu Tiba Asili, Tiba Mbadala, Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Taaluma hiyo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Aidha, Wizara inasisitiza juu ya wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha matangazo yote ya Tiba Asili na Tiba Mbadala yanayotolewa katika vyombo vyao yameidhinishwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Wizara inaangalia uwezekano wa kurekebisha sheria ili kufuta matangazo ya Tiba Asili na Tiba Mbadala.

**HUDUMA ZA DAWA**

***89.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika suala zima la upatikanaji wa dawa kwa kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa,

vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa katika hospitali za rufaa za kitaifa, kanda na za mikoa unaboreshwa, Serikali imefanya mapitio ya kina ya mfumo wa ununuzi, utunzaji na usambazaji katika Bohari ya Dawa kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa dawa.

***90.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeandaa nyezo ijulikanayo kama *PilferageTool* itakayotumika kufanya ukaguzi wa upotevu wa dawa unaosadikika kutokea kuanzia mzigo unapoingia bandarini mpaka kumfikia mgonjwa au mtumiaji wa mwisho. Nyezo hiyo iko katika hatua za majaribio na itaanza kutumika hivi karibuni. Pia, katika kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinapata dawa kwa wakati, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi **420** kutoka hospitali **140** kuhusu uagizaji wa dawa kutoka Bohari ya Dawa kwa njia ya kielektroniki. Katika mwaka 2016/17, hospitali **117** zilizobaki zitapatiwa mafunzo hayo. Wizara itatoa mafunzo, kusambaza na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa ufanisi wa kazi kupitia mfumo wa 5S Kaizen TQM ili kuimarisha usimamizi wa takwimu za dawa.



***91.*** ***Mheshimiwa Spika***, Ili kuepuka kulipa kodi na tozo zilizo juu kutokana na misaada inayoletwa nchini bila ya kuwa na utaratibu maalumu wa kupokea misaada hiyo, Wizara yangu imefanya mapitio ya Mwongozo wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi vya msaada *Donation Guideline* ya mwaka 1995 ili uendane na hali halisi ya sasa. Mwongozo huo upo tayari na umeanza kutumika.

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Bohari ya Dawa imewashirikisha washitiri binafsi **13** katika kanda za Dar es Salaam, Mbeya, Iringa, Moshi, Mtwara na Dodoma. Ushirikishwaji wa washitiri binafsi umesaidia kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa. Aidha, Bohari ya Dawa imempata mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa mikataba mahususi ya kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya uzalishaji wa dawa nchini. Vilevile, Bohari ya Dawa inatumia mfumo wa kufupisha mzunguko wa usambazaji wa dawa kwa kutumia king'atuzi cha *Supply Chain Guru.*

***93.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Bohari ya Dawa itaboresha upatikanaji wa dawa kwa vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuzipa uwezo zaidi Bohari za kanda kujiendesha kimkakati. Hatua hiyo, itaenda sambamba na utumiaji wa washitiri wakubwa

na ufungaji wa mfumo wa kompyuta wa kusajili dawa kwa kutumia ***Bar Code*** katika maghala yake yote. Lengo ni kuongeza ufanisi katika utunzaji na usambazaji wa dawa nchi nzima. Aidha, katika kupunguza fedha za uendeshaji wa Bohari ya Dawa, jumla ya mita za mraba **11,433** ambazo zilikuwa zimekodishwa kwa gharama kubwa zitaachiwa, baada ya **Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kuiwezesha MSD kupata kiwanja chenye ukubwa wa **hekari tano** eneo la Luguruni, Dar es Salaam. Mkakati huo wa kutopanga maghala hayo utaokoa takribani shilingi **bilioni nne** na **nusu** kwa mwaka.

***94.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17, Bohari ya Dawa itaendelea kufungua maduka ya dawa katika hospitali **10** nchini kwa kushirikiana na hospitali husika. Aidha, Bohari itaendelea kuendesha maduka ya dawa katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa Mbeya, Sekou Toure, Mount Meru na Wilaya ya Chato ili yawe mfano katika uendeshaji maduka ya kutolea huduma za dawa katika hospitali zote nchini. Vilevile, Bohari itaanza kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Hatua hiyo itawezesha upatikanaji wa dawa nyingi zaidi kwa gharama nafuu.



## HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

***95.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka, 2015/16, Wizara imetayarisha Mpango Mkakati kwa ajili ya huduma za Uuguzi na Ukunga. Lengo la Mpango huo ni kutoa dira ya huduma za Uuguzi na Ukunga nchini. Aidha, Wizara, imetayarisha mwongozo wa usimamizi shirikishi unaojumuisha suala la utoaji mafunzo kazini. Katika mwaka, 2016/17, Wizara itaandaa mwongozo utakaoelekeza mahitaji halisi ya wauguzi na wakunga kwa kila aina ya Kituo cha kutolea huduma za afya pamoja na aina ya huduma inayotolewa.

## UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

***96.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia ubora wa huduma za afya zinazotolewa nchini. Katika mwaka 2015/16, Wizara imefanya tathimini ya ubora wa huduma katika vituo vyote vinavyotoa huduma za afya ya msingi katika mikoa **20** ya Geita, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Dar es Salaam, Pwani, Singida, Tanga, Manyara, Tabora, Rukwa, Mtwara, Lindi, Morogoro, Ruvuma, Dodoma na Katavi. Vituo vilivyofanyiwa tathmini vimepewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma

zinazotolewa. Jumla ya vituo **5,235** vimefanyiwa tathmini, kati ya vituo hivyo, vituo **2,016** sawa na asilimia 38.51 vimepata nyota sifuri (0), vituo **2,583** sawa na asilimia 49.34 vimepata nyota moja, vituo **561** sawa na asilimia 10.72 vimepata nyota mbili, vituo **68** sawa na asilimia 1.30 vimepata nyota tatu na vituo **vitano** sawa na asilimia 0.10 vimepata nyota nne. Lengo ni kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya vituo vilivyofanyiwa tathmini vinapata nyota 3 au zaidi ifikapo mwezi Juni, 2018. Aidha, tathmini iliyofanywa imeonesha kuwa vituo vinahitaji maboresho ili kutoa huduma stahiki na mipango ya maboresho hayo kwa kila kituo imeandaliwa na kuanza kutekelezwa kwa kutumia Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri.

***97.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya usimamizi shirikishi katika mikoa yote **26** Ili kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa kwenye vituo zinazingatia viwango na miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mipango ya uimarishaji wa utoaji wa huduma bora katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kwa kufanya usimamizi shirikishi na kufanya tathimini ya marudio. Vilevile, Wizara itafanya ukaguzi maalumu wa huduma za afya kwenye vituo endapo kutakuwa na taarifa za kuwepo na ukiukwaji wa maadili na taratibu za utoaji huduma.



***98.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imetoa mafunzo ya kukabiliana na Dharura na Maafa kuhusu huduma za dharura kwa majeruhi wengi kwa wataalamu wa afya katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya na Iringa. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za afya katika dharura na majanga yaliyotokea hapa nchini yakiwemo mafuriko na ajali za barabarani.

***99.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ugonjwa wa kipindupindu umedumu kwa takriban miezi 7 kuanzia mwezi Agosti, 2015, ambapo hadi Aprili, 2016, jumla ya waathirika **21,059** waliugua ugonjwa huo, na kati yao watu **331** wamepoteza maisha. Hadi sasa ni mikoa miwili tu ya Njombe na Ruvuma ambayo haijaathiriwa na ugonjwa huo. Katika kukabiliana na ugonjwa huo, Wizara imeimarisha uratibu na utoaji dawa, vifaa na wataalamu kwenda katika mikoa iliyoathirika kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya juu ya kukabiliana na ugonjwa huo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya vyoo, usafi wa mazingira na umuhimu wa kutumia maji safi na salama.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara kwa kupitia mabaraza ya taaluma ilisimamia maadili na kusajili wataalam waliokidhi viwango vya kutoa huduma za afya nchini. Mabaraza hayo ni pamoja na Madaktari na Madaktari wa Meno, Uuguzi na Ukunga, Famasia, Maabara, Upeo wa Macho Kuona na Afya ya Mazingira. Kupitia usajili unaofanywa na mabaraza mbalimbali ya afya, jumla ya wataalam **54,834** wa kada mbalimbali za afya walisajiliwa. Wataalam hao wakiajiriwa watapunguza pengo lililopo la mahitaji ya watumishi nchini. Aidha, ili kuongeza idadi ya wataalam katika sekta ya afya, Wizara imesajili vyuo **8** vya mafunzo ya uuguzi na ukunga na vyuo **viwili** vya Famasi katika ngazi ya cheti (astashahada)

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imewasajili waganga wa tiba asili na tiba mbadala **2,935** kutoka mikoa yote nchini na hivyo kufikisha waganga **10,958** waliosajiliwa**.** Hii ni hatua muhimu katika kutokomeza vitendo vya ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino, wazee na watoto wachanga vinavyochochewa na imani hatarishi za kishirikina/uchawi. Aidha, Baraza lilifanya ufuatiliaji wa huduma za tiba asili katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Geita,



Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Kagera, Mtwara na Lindi na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo mbalimbali kwa waratibu **75** wa mikoa hiyo pamoja na baadhi ya waganga **890** wa tiba asili.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi nchini, imeendelea kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kusajili vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya. Katika mwaka 2015/16, Wizara kupitia Bodi ya Ushauri ya Uongozi wa Hospitali Binafsi ilisajili vituo vya kutolea huduma za afya **36**, Makampuni na Mashirika **14** yasiyo ya Kiserikali yalisajiliwa kutoa huduma za Afya, hivyo kufikia jumla ya vituo **1,927** kati ya vituo **7,285** vya kutolea huduma za afya. Vituo hivyo binafsi ni sawa na asilimia **26.45** ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ilisajili maabara binafsi za afya **60,** hivyo kufikia jumla ya maabara binafsi **647** kati ya maabara **4,852**. Maabara binafsi ni sawa na asilimia **13.33** ya maabara zote za kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, Baraza la Uuguzi na Ukunga limesajili vituo vipya **12** vya huduma binafsi za uuguzi na ukunga na hivyo kufikisha jumla ya vituo kuwa **90**.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Baraza la Famasi limesajili Maduka ya Dawa Moto **163** na kufikia jumla ya maduka ya dawa moto **1,104**, Maduka ya Dawa Muhimu (ADDO) **770** na kufanya jumla ya ADDO nchini kuwa **9,100.** Serikali imezingatia umuhimu wa kusogeza huduma za upatikanaji wa dawa kupitia sekta binafsi karibu na wananchi. Baraza la Optometria limesajili optometri kliniki **12**, na vituo vya kutengeneza miwani tiba **vinne** na duka **moja** linalouza vifaa vya Optometri. Jumla ya kliniki za Optometri katika hospitali za umma ni **87**, hospitali binafsi ni **146** na hivyo kufikia vituo **233** na maduka yanayouza vifaa vya Optometri kuwa **tisa**.



## URATIBU, UFUATILIAJI NA UGHARAMIAJI HUDUMA ZA AFYA

### Uratibu na Ufuatiliaji Huduma za Afya

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya sekta ya afya, Wizara imeendelea kutekeleza utaratibu wa kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card) kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Tathmini hiyo imeendelea kufanyika katika zahanati na vituo vya afya vya Serikali vya Halmashauri za Wilaya **23** za Mikoa ya Shinyanga (4), Mwanza (5) Geita (5), Simiyu (5) na Pwani (4) (**Kiambatisho.4).**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa katika sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanya usimamizi shirikishi katika Bodi **44** za Halmashauri za Huduma za Afya. Usimamizi huo ulizingatia uwepo wa Hati Rasmi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi na kamati za usimamizi za vituo vya afya.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeboresha upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani "Health Facility Registry". Mfumo huo unamuwezesha mwananchi kupata taarifa za sifa ya kituo, huduma zinazotolewa, taarifa za kijographia, na aina ya kituo. Taarifa hizo zinapatikana kwa njia ya mtandao kwa anuani ya ***ehealth.go.tz***. Wizara pia, imezindua mtandao wa kutoa taarifa za takwimu za afya kupitia anuani ya ***hmisportal.moh.go.tz.***

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wa ehealth strategy 2013-2018. Katika mwaka 2015/16, Wizara imesambaza mwongozo wa ufungaji wa mfumo wa kielektroniki na miundombinu yake katika Hospitali na Vituo vya Afya. Mwongozo huo unatoa maelekezo kuhusu sifa, ubora na viwango ambavyo mfumo wa kielektroniki unatakiwa kukidhi. Aidha, Wizara ilikamilisha kufunga mfumo wa kielektroniki katika Hospitali Maalumu ya Kibong'oto, Mirembe na hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Amana, Ndanda, Lindi na Mount Meru. Vilevile, Wizara imekamilisha kutengeneza mfumo wa kielekroniki wa kuandaa mipango na matumizi katika halmashauri unaojulikana kama "centralized web



based PlanRep" na kukamilisha kufanya tathmini ya tiba mtandao (telemedicine) katika hospitali saba za Bagamoyo, Amana, Mwananyamala, Hydom, Tumbi, KCMC na Hospitali ya Taifa Muhimbili zilizokuwa katika majaribio ya kutoa huduma hiyo.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya tathmini ya mifumo iliyofungwa ya kielektroniki ya kukusanya mapato na taarifa za hospitali katika hospitali za rufaa za Kanda, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi viwango, sifa na ubora kwa mujibu wa miongozo ya Wizara yangu na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA). Tathmini hiyo itawezesha Wizara kutoa bei elekezi ya kufunga na kuendesha mifumo ya kielektroniki ili kuhakikisha mifumo hiyo haiongezi gharama kwa mgonjwa na kuboresha huduma.

**109.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2016/17, Wizara itafunga mfumo wa kielektroniki unaoitwa "*Integrated Health Facility Management Information System" (iHMIS)* katika Taasisi ya Huduma ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali ya Benjamin Mkapa (Dodoma), hospitali za rufaa za mikoa ya Tabora (Kitete), Singida, Tanga (Bombo), Mtwara (Ligula), Mwananyamala na Temeke. Aidha, Wizara itakarabati vifaa vya tiba mtandao (telemedicine) katika Hospitali ya Taifa

Muhimbili, Hospitali za kanda Bugando, KCMC na Mbeya, hospitali za rufaa za mikoa za Mwananyamala, Temeke, Amana, Tumbi na Hospitali ya Halmashauri ya Bagamoyo. Vilevile, Wizara itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa kutumia simu ya kiganjani (mHealth) kwa wananchi ili kutoa taarifa za ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.

**Ugharamiaji wa Huduma za Afya**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati wa Ugharamiaji huduma za afya ambao una lengo la kutafuta vyanzo mbalimbali vya uhakika vya kuongeza raslimali fedha katika Sekta. Nia ni kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma za afya bila kuwa na kikwazo cha fedha pindi wahitajipo huduma za afya.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa wananchi wote wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha wala kujali hali yao ya kiuchumi katika jamii. Aidha, Sera imesisitiza uwepo wa vyanzo vya fedha vinavyoaminika pamoja na kuhakikisha sekta ya afya inapata raslimali za kutosha za kugharamia huduma za afya. Katika kutekeleza matakwa ya Sera hiyo, Wizara imekuwa ikibuni na



kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. Hadi kufikia Desemba 2015, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Jamii (CHF) ulikuwa unahudumia jumla ya **wanufaika 11,729,281** sawa na asilimia **27** ya Watanzania wote kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Kati ya hao wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii ni **8,390,526** na wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni **3,338,755** (**Kiambatisho Na. 5).** Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali za kuhamasisha jamii kujiunga na huduma za Mifuko hiyo zilizowezesha kuongezeka kwa wanachama walioandikishwa kutoka makundi mbalimbali kama; vikundi vya wajasiriamali na ushirika, wanafunzi, Taasisi za kidini, na mashirika binafsi.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za Mfuko kwa wanachama wake zimeendelea kuboreshwa, Hadi tarehe 31 Desemba, 2015 Mfuko umeanzisha kituo cha huduma kwa wateja (**Simu na 0800 110063 bila malipo).** Huduma hiyo itawawezesha wananufaika kutoa kero na maoni yao kwa mfuko kwa haraka na bila kikwazo cha malipo. Aidha, Mfuko umevilipa vituo vilivyotoa huduma kwa wanufaika wa Mfuko kiasi cha **shilingi 101,772,424,344.00** (**Kiambatisho Na. 6**). Vilevile, Mfuko umeanza kutoa kwa mara ya

kwanza, huduma za upasuaji wa moyo na uzibuaji wa mishipa ya damu kwa wanachama wa Mfuko katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete. Fao hilo limewezesha kupunguza idadi ya wagonjwa wanaoenda nje ya nchi na kuimarisha matibabu ya ndani. Aidha asilimia 80 ya kazi za uendeshaji wa Mfuko zinafanywa kupitia mifumo habari (TEHAMA) iliyosaidia sana utambuzi wa wanachama kabla ya kupata huduma na kuwalipa watoa huduma kwa wakati kwa mujibu wa Sheria.

113. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Mpango wa Afya ya Jamii Mijini –Tiba kwa Kadi (TIKA), Halmashauri za Manispaa za Tabora, Kigoma Ujiji na Morogoro; Halmashauri za miji midogo za Kibaha, Kasulu, Geita, Mpanda, Njombe, Makambako na Babati zimeanzisha huduma ya Tiba kwa Kadi. Aidha, Halmashauri za Uvinza, Buhigwe, Itigi na Mkalama zimeridhia uanzishwaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kufanya jumla ya halmashauri zote zinazotekeleza huduma ya Mfuko wa Afya ya Jamii CHF/TIKA kufikia **151** kati ya **182**. Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na kwa kushirikiana na Wadau, imeendelea kuuboresha Mfuko wa Afya ya Jamii kwa lengo la kuongeza ufanisi wake na huduma zake kwa wananchi.



114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, utafanya Tathimini ya Tano ya Uhai wa Mfuko *(Actuarial Valuation)*, ili kuangalia uwezo wa Mfuko kuhimili utoaji wa huduma kwa kipindi kirefu kijacho. Maandalizi ya kazi yamekwisha anza na moja kati ya Hadidu Rejea itakuwa ni kuangalia namna bora ya kuunganisha huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, utaanza kugharamia huduma za matibabu kwa Watoto wenye umri chini ya miaka 18 bila kuangalia uhusiano uliopo kati ya mtoto na mchangiaji. Hatua hiyo inakusudia kuongeza wigo wa walengwa na kuwawezesha watoto walio katika familia kubwa au wanaolelewa na walezi nje ya wazazi wao ikiwemo wale wanaoishi katika mazingira magumu kupata huduma za Mfuko.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa Waheshimiwa wabunge wote, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujiunga na bima ya afya. Aidha, naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inatarajia kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Bima ya Afya. Muswada huo una mapendekezo mbalimbali ikiwemo sharti la ulazima wa wananchi

wote kujiunga na Bima ya Afya na wale wote wenye uwezo kuchangia bima hiyo. Ni mategemeo yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtaunga mkono jitihada hizo za Serikali na kupitisha Muswada huo pindi utakapowasilishwa.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeanzisha mfumo wa kuimarisha sekta ya afya kwa kuvipatia fedha vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kulingana na ubora wa huduma wanazozitoa kwa wananchi. Mpango huo unaitwa malipo kwa ufanisi (Results Based Financing - RBF). Lengo ni kuviwezesha vituo kupata fedha za kuboresha utoaji wa huduma na vilevile kutoa motisha kwa watumishi kutokana na utendaji wao. Utekelezaji wa Mpango huo ulianzia katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwaka 2015 ambapo kuanzia Januari 2016 Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga zimeshaingizwa katika mpango huo na Mkoa wa Mwanza umeanza utekelezaji Aprili 2016. Aidha, Mfumo huo umeanza kuonesha manufaa katika vituo husika kwa kuongezeka kwa utumiaji wa huduma za afya za msingi na ubora wa utoaji wa huduma hizo. Ubora huduma umeongezeka kutoka **asilimia 48** hadi **64** kwa kipindi cha Aprili hadi Desemba 2015 kwa Halmashauri ya Kishapu.



**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kuingiza mikoa mingine minne katika Mpango wa RBF. Mikoa hiyo ni Pwani, Simiyu, Tabora na Kigoma. Mikoa hiyo imepewa kipaumbele kutokana na mahitaji makubwa yaliyobainishwa na viashiria vya afya katika Mikoa hiyo. Hata hivyo, Mikoa mingine itaendelea kuongezwa katika utaratibu huo kulingana na upatikanaji wa fedha.

## UDHIBITI WA KEMIKALI NCHINI

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa 2015/16, Wakala imepata ithibati ya maabara kwa kiwango cha kimataifa cha "ISO 17025:2005" ya Maabara ya Ubora wa Vyakula kwa vigezo vya SADCAS na imekarabati jengo la Kanda ya Mashariki lililopo makao makuu Dar es Salaam, hivyo kuimarisha uwezo wa nchi katika kufanya uchunguzi wa ubora wa vyakula. Katika mwaka 2016/17, Wakala itakamilisha zoezi la kupata hati ya ithbati ya maabara katika kiwango cha kimataifa cha "ISO 17025:2005" kwa maabara ya vinasaba vya binadamu (DNA).

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya sampuli **4,121** zilizofanyiwa uchunguzi na

matokeo kutolewa. Sampuli zilizochunguzwa ni za vyakula, dawa, kemikali, maji na maji taka, bidhaa za viwandani na mazingira, za makosa ya jinai na matatizo ya kijamii. Aidha, Wakala ilitoa elimu kwa wadau **359** kutoka katika taasisi mbalimbali nchini zikiwemo za sekta binafsi juu ya taratibu sahihi za uingizaji, utunzaji, na usafirishaji wa kemikali pamoja na matumizi salama ya kemikali ili kulinda afya na mazingira. Wadau **402** wanaohusika na biashara ya kemikali walisajiliwa na maeneo **650** yalikaguliwa. Vilevile, Wakala ilitoa mafunzo kwa wadau **56** ya kukabiliana na ajali zinazohusika na Kemikali

**120.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Aidha, Wakala ilifanya ukaguzi wa mizigo ya kemikali **14,578** iliyopita katika bandari, bandari kavu, na viwanja vya ndege ambapo mizigo iliyokidhi viwango iliruhusiwa kuingia nchini. Katika mwaka 2016/17, Wakara itaendelea kufanya ukaguzi wa mizigo ya kemikali inayoingia nchini.



## UDHIBITI WA UBORA WA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua maeneo **6,896** yanayohusika na uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo ambapo maeneo **4,515** sawa na asilimia **65** yalikidhi vigezo. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na ya kusindika chakula na sehemu **3,718** za kuuzia chakula**;** maduka **954** ya dawa**;** vituo vya afya **414**; maduka **1,406** ya vipodozi**;** maduka **316** ya vifaa tiba**;** viwanda **70** vya dawa nje ya nchi; viwanda **12** vya dawa vya ndani**;** na viwanda **6** vya vipodozi. Maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya Sheria, wamiliki walielekezwa kufanya marekebisho husika ndani ya muda maalum.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2015/16 Mamlaka ya Chakula na Dawa ilisajili na kuhuisha vibali vya maeneo **3,186** ya kufanyia biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Aidha, Mamlaka ilitathmini maombi **4,207** ya kusajili bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ikiwa ni sawa na **asilimia 85** kati ya maombi **5,083** yaliyopokelewa. Jumla ya maombi **2,747** sawa na asilimia **65** ya maombi yote yaliyofanyiwa tathmini yalisajiliwa. Vilevile, Mamlaka

ilitoa vibali **5,705** vya kuingiza bidhaa nchini na **1,179** vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

***123.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Jumla ya tani **226.8** zenye thamani ya **Shilingi 1,983,230,330** ziliteketezwa ambapo vipodozi ni tani **66.8** sawa na asilimia **29.5**; vyakula ikijumuisha pombe bandia aina ya viroba tani **145.37** sawa na asilimia **64.1;** dawa tani **14.48** sawa na asilimia **6.4** na vifaa tiba tani **0.15** sawa na asilimia **0.1**. Aidha, Mamlaka ilichunguza sampuli **2,736** za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo sampuli **2,567** ikiwa ni sawa na asilimia **94** zilikidhi viwango vya ubora na usalama. Bidhaa zote ambazo hazikukidhi viwango aidha zilizuiliwa kuingizwa nchini au zile zilizokutwa sokoni ziliondolewa na matumizi yake kusitishwa. Pia, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kupitia radio, luninga, magazeti na mikutano. Jumla ya vipindi **22** vya radio na luninga vilirushwa hewani na mikutano ya wazi **29** ikihusisha makundi mbalimbali ikiwemo wanafunzi wa vyuo na mashuleni ilifanyika.

***124.*** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Mamlaka itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba nchini. Aidha, Mamlaka itaimalisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuboresha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na kufuatilia malalamiko ya wateja, kuyapatia ufumbuzi na kutoa mrejesho kwa wakati. Pia, elimu kwa umma itaendelea kutolewa kwa lengo la kujenga uwezo wa wananchi kutambua bidhaa duni na bandia na hivyo kutoa mchango katika udhibiti. Vilevile, Mamlaka inatarajia kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Ofisi na Maabara ya Kanda ya Ziwa katika jiji la Mwanza lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

**UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU**

***125.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu iliendelea na utafiti unaolenga kubaini kiwango cha maambukizi ya kichocho na minyoo ya tumbo katika Wilaya za Rorya na Butiama mkoani Mara. Matokeo ya awali yanaonesha kwamba ugonjwa wa kichocho cha tumbo ni tatizo kubwa la kiafya katika wilaya zote mbili. Katika mwaka 2016/17, Taasisi itafanya utafiti utakaotathmini kama chanjo moja dhidi ya virusi vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi

(Human Papilloma Virus, (HPV)) itakuwa na uwezo wa kutengeneza kinga mwilini sawa na chanjo mbili au tatu. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti wa awali wa kuangalia ubora na usalama wa chanjo dhidi ya virusi vya Ebola. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Kikundi cha Kudhibiti UKIMWI mkoani Tanga (TAWG), itafanya majaribio juu ya ubora na usalama wa dawa asili aina ya TASHACK ya tiba ya UKIMWI ambayo imeboreshwa na kutengenezwa kiwandani.



## B: MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

### Maendeleo ya Jamii

***126.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Wizara yangu iliendelea kuratibu utekelezaji wa majukumu ya maafisa maendeleo ya jamii kwa kutoa elimu na kuchochea ari ya wananchi ya kujiletea maendeleo yao wenyewe na ya taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii imehamasisha wazazi na walezi haki ya kuwaendeleza watoto kielimu ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusu uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi inaonesha kuwa wananchi wamehamasika na kuwapeleka watoto shule na kufanya lengo la uandikishaji katika shule za msingi kufikia **asilimia 119.5.** Pamoja na jitihada hizo za Maafisa Maendeleo ya Jamii, bado kuna upungufu mkubwa wa wataalam hao katika ngazi ya Kata ambapo kati ya Kata **3,957** zilizopo nchini, ni Kata **1,332** pekee ndizo zenye wataalam hao na Kata **2,625** hazina wataalam hao kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 7.** Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kutoa hamasa kwa jamii kujiletea maendeleo jumuishi ikiwa ni pamoja na kuwapeleka watoto shule bila kujali jinsia, hali ya ulemavu au uwezo wa kiuchumi wa wazazi.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia azma ya **Mheshimiwa Rais Dr. John Pombe Joseph Magufulu** ya kujenga ari ya kufanya kazi kwa watanzania, katika mwaka 2015/16 Wizara yangu kupitia vyombo vya habari ilihamasisha jamii kujenga ari ya kufanya kazi kwa bidii na kujiletea maendeleo. Mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia vyombo vya habari na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya halmashauri na mkoa itaendelea kutoa hamasa kwa wananchi kupenda kufanya kazi.

### Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni chachu katika kuwezesha jamii kujiletea maendeleo. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kusimamia taaluma hiyo na kuzalisha wataalam hao kupitia vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii (**Kiambatisho Na.8**) na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (Arumeru). Taaluma hiyo inatolewa katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya uzamili. Katika mwaka 2015/16, jumla ya wanachuo **2,130** (Ke: 1,270, Me: 860) walidahiliwa katika fani ya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanachuo **3,594** waliodahiliwa mwaka 2014/15



ikiwa ni pungufu ya asilimia **48.** Upungufu huu umesababishwa na uchakavu wa majengo na miundombinu. Kupungua kwa udahili katika vyuo kutasababisha upungufu wa wataalam wenye ujuzi wa taaluma ya maendeleo ya jamii katika jamii. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuvutia vijana wengi kujiunga na vyuo hivyo. Aidha, Wizara imetenga kiasi cha **shilingi milioni 200** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi kwa ajili ya kutatua mgogoro wa ardhi katika chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

### Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imewezesha utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Wananchi na Ufundi Stadi kwa wananchi **24,619** (Me:12,563, Ke: 12,056) kupitia vyuo **55** vya maendeleo ya wananchi (**Kiambatisho Na. 9**). Kati yao, wananchi **4,353** (Me:2,983, Ke: 1,370) walipata mafunzo ya Ufundi Stadi ikilinganishwa na wananchi **4,288** waliopata mafunzo hayo mwaka 2014/15 na wananchi **2,758** (Me:1,847, Ke:911) walipata mafunzo ya Elimu ya Wananchi ikilinganishwa na wananchi **3,818** ambao walipata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Aidha, mafunzo ya

muda mfupi yalitolewa kwa wananchi **13,570** (Me: 5,906, Ke: 7,664) ikilinganishwa na wananchi **8,875** ambao walipata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Kadhalika, mafunzo nje ya vyuo yalitolewa kwa wananchi **2,816** (Me: 1,270, Ke: 1,546) ikilinganishwa na wananchi **1,281** waliopata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Katika mwaka 2016/17 Serikali inatarajia kupima maeneo ya vyuo, kufanya ukarabati wa miundombinu na kuzalisha wahitimu **2,400** wa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda, ajira na maendeleo ya jamii.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** elimu ya awali imeendelea kutolewa kwa watoto wadogo kupitia vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyopo katika Vyuo **36** vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya watoto wadogo **1,122** (wavulana 557 na wasichana 565) walipata mafunzo ya malezi na makuzi kwa watoto chini ya miaka mitano, ikilinganishwa na watoto **909** waliopata mafunzo kama hayo mwaka 2014/15. Vilevile, vifaa vya michezo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaopata Elimu ya Awali vilitolewa katika vituo **55** vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mwaka 2016/17,



Wizara itaendelea kutoa elimu ya awali kupitia vyuo hivyo ambapo jumla ya watoto **1,650** wanatarajiwa kudahiliwa.

**Maendeleo ya Jinsia**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa hapa nchini, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/16 na mpango wa mwaka 2016/17 umegawanyika katika maeneo yafuatayo:

**Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera na Mipango**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mipango, mikakati, programu na bajeti ni muhimu katika kuhakikisha masuala hayo yanazingatiwa ipasavyo ili kuondoa tofauti za kijinsia nchini. Mwaka 2015/16 Wizara kupitia Kikosi Kazi cha Uingizaji wa Masuala ya Jinsia katika Sera za Kitaifa iliwezesha uingizaji wa masuala ya jinsia katika Hadidu za Rejea za kufanya mapitio ya utekelezaji wa MKUKUTA II.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Wizara yangu iliendelea kuratibu madawati ya jinsia katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Madawati haya ni muhimu katika kufanya uchambuzi wa kijinsia na kuingiza masuala ya jinsia kwenye sera, mikakati, mipango, programu na bajeti katika sehemu ya kazi. Hata hivyo, utendaji wa madawati haya unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti na vitendea kazi. Naomba nitoe wito kwa Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara, Wakala, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kutenga rasilimali fedha na kuyapatia madawati haya vitendea kazi pamoja na kuyashirikisha katika maandalizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuratibu uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera za Kitaifa hasa katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21). Wizara pia itahuisha uingizaji wa masuala ya jinsia kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo Endelevu (2030) na Agenda ya Afrika Tuitakayo 2063 inayolenga kufikia maendeleo jumuishi katika jamii. Vilevile Wizara itakuwa inatambua mchango wa Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali ili kuhamasisha na kujenga ari katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Mikakati yao.



**Ukatili wa Kijinsia**

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kwa jamii dhidi ya ukatili wa kijinsia. Waathirika wa ukatili huo mara nyingi ni wanawake na watoto ambapo huwasababishia madhara ya kimwili, kisaikolojia, kiafya na kiuchumi. Takwimu zinaonesha kuwa ukatili wa kijinsia bado ni tatizo kubwa hapa nchini ambapo kati ya Januari hadi Disemba 2015, matukio **22,876** yameripotiwa. **(Kiambatisho Na. 10).** Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kusimamia sheria na kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia.

**Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano ni kuwawezesha wanawake kiuchumi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeendelea kuratibu utendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuwainua kiuchumi.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Benki ya Wanawake Tanzania imetoa mafunzo ya ujasiriamali

na mikopo kwa wananchi **12,874** wakiwemo wanawake **9,693** (1,485 wakiwa ni wanawake wa vijijini) na wanaume **3,181.** Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya **shilingi 20,124,874,328** zilikopeshwa ambapo wanawake walipata mikopo yenye thamani ya **shilingi 12,878,977,228** na wanaume mikopo yenye thamani ya **shilingi 7,245,897,100.** Mikopo hiyo, imewawezesha wanawake wajasiriamali wadogo wadogo kujiajiri katika shughuli mbalimbali za biashara, kilimo na ufugaji na hivyo kuinua vipato vyao na vya familia. Katika mwaka 2016/17, Benki ya Wanawake Tanzania inatarajia kufungua dirisha maalum la kutoa mikopo yenye riba nafuu ili kuwafikia wanawake wengi zaidi.

***137.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake chini ya Wizara umetoa jumla ya **shilingi milioni 54** kwa Halmashauri **7** za Chato, Kaliua, Busega, Uvinza, Wanging'ombe, Mkalama na Momba. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya mfuko ambayo inaonesha pamoja na mambo mengine kuwa kuna mwitikio mdogo wa halmashauri kuchangia asilimia tano kama zinavyotakiwa (**Kiambatisho Na.11**). Aidha, kwa kutumia mapendekezo ya tathmini hiyo Wizara iliandaa mkakati wa kuboresha usimamizi, uendeshaji na uratibu wa mfuko. Mwaka



2016/17, Wizara itaendelea na usimamizi na uratibu wa utoaji wa mafunzo, mikopo, urejeshaji na kuhakikisha halmashauri zinachangia asilimia tano kutoka katika vyanzo vya mapato ya halmashauri.

***138.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa **Mheshimiwa Ban Ki Moon** kuwa mjumbe wa jopo la ngazi ya juu la Umoja wa Mataifa la kuwawezesha wanawake kiuchumi**.** Uteuzi huu unakuja wakati Wizara yangu inaandaa mikakati ya kuongeza jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi hasa katika kupata huduma za kifedha. Tafiti za matumizi ya huduma za kifedha hapa nchini zinaonesha kuwa wanawake wachache sawa na **asilimia 51.2** wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na wanaume sawa na **asilimia 63.** Aidha, tafiti zinabainisha kuwa wanawake wanaomiliki simu za kiganjani ni wachache sawa na **asilimia 53.2** ikilinganishwa na wanaume sawa na **asilimia 70.5.** Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itashirikiana na Mhe. Makamu wa Rais katika kutimiza dhamira yake ya kuanzisha kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha na kuwawezesha wanawake kufungua akaunti za Benki

na kutumia Benki Mtandao. Naamini kwa kufanya hivyo wanawake wengi wataweza kutumia Benki Mtandao kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo VICOBA na SACCOS. Sambamba na hilo Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake kutumia Taasisi za Kifedha zikiwemo SACCOS na VICOBA ili kuhakikisha kuwa wanawake wengi wanapata fursa za kukopa na kujiwekea akiba na hivyo kuondokana na umaskini.

**Maendeleo ya Watoto**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2015/16 Wizara iliandaa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto na kuiwasilisha kwa Kamati ya Umoja wa Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto mwezi Julai, 2015. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitekeleza mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto. Taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, ilibainisha kuendelea kuwepo kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni hasa katika mikoa ya Mara, Singida, Dodoma, Shinyanga na Geita. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuinua uelewa na uwezo wa jamii kushiriki kikamilifu katika kutokomeza na kuzuia mimba na ndoa za utotoni katika halmashauri 29 kutoka mikoa yenye kiwango cha juu.



**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Wizara iliwajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii katika wilaya **64** kuhusu zana ya mawasiliano ya elimu ya malezi ya familia na kusambaza nakala **2,000** za kitini cha elimu ya malezi kwa familia kwa ajili ya kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Mafunzo hayo yamesaidia kuongeza uwezo wa jamii kubaini na kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili. Mfano, utoaji wa taarifa kupitia mtandao wa simu wa watoto 116 uliongozeka kutoka **24,675** mwaka 2014/15 hadi kufikia **33,675** mwaka 2015/16. Mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wa matumizi ya kitini hicho Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri **27** nchini. Vile vile, Wizara itaendelea kuelimisha wazazi, walezi na jamii kutoa taarifa punde vitendo vya ukatili vinapotokea na kuratibu uhamasishaji wa utoaji elimu ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto kupitia kipindi cha walinde watoto kinachorushwa na radio jamii **19** zilizopo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukeketaji ni miongoni mwa vitendo vya ukatili vinavyochochewa na mila na desturi zenye kuleta madhara kwa watoto wa kike. Katika kukabiliana na tatizo hilo mwaka 2015/16 Wizara ilihamasisha jamii kuhusu madhara ya

ukeketaji ikiwa ni pamoja na vifo vya watoto wa kike. Aidha, jamii ilihamasishwa kuachana na ukeketaji na kushiriki kikamilifu katika kupinga vitendo hivyo. Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufuatilia na kuelimisha jamii kuachana na ukeketaji.

***142.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha haki ya mtoto ya kuendelezwa hasa kwa mtoto wa kike, mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwapatia elimu watoto wa kike sawa na watoto wa kiume. Vilevile, Wizara imehamasisha jamii na wadau mbalimbali kujenga mazingira mazuri ya wasichana kuendelea na masomo. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha jamii na wadau wa maendeleo kuboresha mazingira ya shule kuwa rafiki kwa watoto wa kike. Aidha, itahamasisha uanzishwaji wa klabu za wasichana shuleni zitakazo wasaidia kujijenga kielimu na kimaisha.

***143.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mabaraza ya watoto ni muhimu katika kuwajengea uwezo wa kujiamini na kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wao. Mwaka 2015/16 mabaraza 5 yalianzishwa na kufanya idadi ya mabaraza hayo kuongezeka kufikia **122** mwezi Machi, 2016 (**Kiambatisho Na. 12**). Napenda kuzihimiza halmashauri ambazo hazina



mabaraza ya watoto kuanzisha mabaraza hayo haraka. Kupitia mabaraza haya, watoto wanapata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali na kuwajengea uwezo wa kujiamini. Nitumie fursa hii kumpongeza **mtoto Getrude Clement** mwenye umri wa miaka 16 aliyeweza kushiriki na kuhutubia kwa kujiamini Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Marekani chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Umoja huo Mheshimiwa Ban Ki Moon. Nawahimiza wazazi/walezi kuwaruhusu watoto wao kujiunga na mabaraza na klabu mbalimbali za watoto. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa mabaraza hayo pamoja na kuhamasisha halmashauri kuyaanzisha na kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kuyaendesha hasa katika ngazi ya halmashauri na kata.

### Maendeleo na Ustawi wa Wazee

***144.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mauaji ya wazee bado ni tatizo kubwa hapa nchini ambapo mwaka 2015/16 jumla ya wazee **167** wameuwa kwa sababu ya imani potofu. Mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ulinzi, matunzo na usalama wa wazee kupitia maadhimisho ya kimataifa ya Siku

ya Wazee Duniani, makongamano na vyombo vya habari. Katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kuwasilisha mswada wa Sheria ya Wazee pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ulinzi, matunzo na usalama wa wazee. Wazee ni hazina tuna wajibu wa kuwalinda, kuwatunza na kuwathamini. Sote ni wazee watarajiwa.

***145.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kutoa matunzo kwa wazee wasiojiweza katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali. Matunzo hayo ni pamoja na huduma ya chakula, malazi na matibabu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya makazi ya wazee na kuboresha upatikanaji wa chakula kwa ajili ya wazee katika makazi.

**Ustawi wa Jamii**

***146.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu, kutoa na kusimamia huduma ya malezi ya kambo na kuasili watoto ambapo jumla ya mashauri **61** yalipokelewa na watoto **35** wapo katika malezi ya kambo, watoto **25** waliasiliwa na maombi 26 bado yanaendelea kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa polisi, taarifa za kimataifa,



uchunguzi wa kijamii, pamoja na kurekebisha taarifa zenye upungufu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuratibu huduma za unasihi, usuluhishi na upatanishi katika mashauri ya ndoa zenye mifarakano na migogoro katika Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

***147.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo vya walezi wa watoto. Jumla ya vituo **28** vya kulelea watoto wadogo mchana na chuo kimoja cha malezi vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo **51** vya kulelea watoto na vyuo **viwili** vya walezi wa watoto vilivyosajiliwa mwaka 2014/15. Jumla ya walezi **1,019** walipatiwa mafunzo ili kuboresha huduma zitolewazo katika vituo hivyo ikilinganishwa na walezi **600** waliopatiwa mafunzo mwaka 2014/15. Mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo vya walezi wa watoto.

***148.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kushirikiana na Manispaa ya Temeke Wizara iliandaa mafunzo kwa wamiliki na walezi **50** wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Kanuni za Vituo vya Kulelea Watoto

Wadogo Mchana na Watoto Wachanga za mwaka 2012 pamoja na namna ya kuanzisha na kuendesha vituo hivyo kwa kuzingatia viwango vya ubora wa huduma katika manispaa husika. Aidha, nakala 1,000 za kadi za ufuatiliaji wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (miaka 0 – 8) zilichapishwa ili kuhamasisha wazazi na walezi kufanya ufuatiliaji wa karibu wa makuzi na maendeleo ya watoto.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Wizara iliendelea kusimamia na kutoa huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto na shule ya maadilisho. Wizara imehudumia jumla ya watoto **346** wakiwemo **327** wanaume na **19** wasichana waliohifadhiwa katika mahabusu za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es Salaam na Shule ya Maadilisho Irambo ikilinganishwa na watoto **357** kati yao, wavulana walikuwa **304** na wasichana **33** waliohudumiwa mwaka 2014/15. Aidha, watoto waliohudumiwa mahakamani katika mwaka 2015/16 ni **164** wakiwemo **133** wanaume na **31** wasichana. Mwaka 2016/17, wizara itaendelea kuelimisha jamii kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. Wizara pia itaendelea kuhudumia mahabusu ya watoto, shule ya maadilisho na makao ya watoto.



**Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilidahili wanafunzi **1,308** ikilinganishwa na wanafunzi **1,376** waliodahiliwa mwaka 2014/15. Katika mwaka 2016/17, taasisi imepanga kudahili wanafunzi **2,280.** Mikakati itakayotumika kuongeza udahili ni kutangaza chuo, kutembelea shule za sekondari zenye kidato cha tano na sita na kuzungumza na wanafunzi kwa kuwashawishi kujiunga na taasisi watakapomaliza elimu ya sekondari. Aidha, taasisi inataraji kufungua matawi ya chuo Mbeya, Mwanza na Arusha.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yashiriki kikamilifu na kuchangia katika kuleta maendeleo ya jamii na taifa. Katika mwaka 2015/16, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **428** yalipatiwa usajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 na kufanya idadi ya mashirika haya kuongezeka kutoka **7,060** mwezi Machi, 2015 hadi kufikia **7,626**

mwezi, Machi, 2016 (**Kiambatisho Na. 13**). Aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **108** yalifutiwa usajili wao kutokana na kukosa sifa za kisheria za kuendelea kufanya kazi. Katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakayokidhi matakwa ya kisheria.

***152.*** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyowasilisha taarifa za mwaka za kazi na fedha imeongezeka kutoka mashirika **187** mwaka 2014/15 hadi kufikia mashirika **375** mwaka 2015/16 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 100.5.** Wizara ilichambua taarifa hizo na kutoa mrejesho kwa mashirika husika. Taarifa za mashirika hayo zinaonesha kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kushiriki katika shughuli za maendeleo hususan masuala ya sera, utawala bora, utoaji huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo mbalimbali ikiwemo elimu, afya, kilimo, ardhi, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, maendeleo ya jinsia, ajira, ustawi wa jamii na maendeleo ya mtoto.

***153.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Serikali itafuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini na kutambua mchango wa mashirika hayo katika maendeleo. Katika kutekeleza hilo, Serikali itapitia taarifa za mwaka za kazi na fedha zinazowasilishwa



na mashirika hayo na kukagua miradi ya mashirika husika katika maeneo ya utekelezaji. Aidha, itaainisha na kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika sekta mbalimbali kwa kuandaa taarifa ya mchango wa mashirika hayo katika maendeleo na kuisambaza kwa wadau kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

***154.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Serikali itawezesha kufanyika kwa tathmini ya Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 ili kupima utekelezaji wake, kuainisha mafanikio yaliyofikiwa, changamoto na fursa zilizopo katika kuiboresha sera husika kwa ajili ya kuyawezesha mashirika haya kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuwahudumia wananchi kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine.

**Uratibu wa Sera, Programu na Mipango ya Wizara**

***155.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2015/16 Wizara iliratibu mipango na programu mbalimbali za Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (Julai 2011-Juni, 2016) na kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (2016/17 – 2020/21) utakaoendana na

Mpango wa Pili wa Maendeleo (2016/17-2020/21) na mabadiliko ya Wizara yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Halmashauri watajengewa uwezo wa kukusanya, kuchambua, kuandaa na kutoa taarifa za sekta ya maendeleo ya jamii kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ulioandaliwa.

## USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda za SADC, EAC, ECSA-HC na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa na katika kutekeleza maamuzi ya pamoja yenye manufaa kwa taifa. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia Wizara yangu. Aidha, itaimarisha ushirikiano na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, Malaria Afrika, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Wazee, Kutotumia Tumbaku, Tiba Asili ya Mwafrika, Wachangia Damu, Utepe Mweupe, Siku ya Wauguzi na Fimbo Nyeupe na Siku ya Mtoto Njiti duniani.



## SHUKRANI

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), na Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, na UNFPA kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, naishukuru na kuipongeza Korea Kusini kupitia shirika lake la Maendeleo (KOICA) kwa kuamua kujiunga na nchi zinazochangia fedha katika Mfuko wa pamoja kwa ajili ya huduma za afya kuanzia mwaka 2016/17. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika ($A_f$DB), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), GAVI, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), UNFPA, UN-Women, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni *Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine* ya Marekani, Canadian Bar Association, *CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work* ya Chuo Kikuu cha *Illinois* Marekani, *John Snow Incorporation (JSI), JICA, KOICA, KfW,Global Partnership for Education (GPE),* Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka *(Medicins Sans Frontieres – MSF),MSERIOR,* ORIO, *P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden)*, Shirika la Upasuaji la *Spain, SIGN* la Marekani, na Shirika la *Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID* na*, Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.*



**159.** ***Mheshimiwa Spika*,** tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorcerciasis Control, *Africare, Axios International, Aids Relief Consortium, AIHA, ASCP, ASM, APHL, Balm and Gillead Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief Services (CRS), Citi Bank, Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), Global Fund to fight AIDS, TB and Malaria (GFATM), General Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm*

*Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital- London, Save the Children, SightSavers International, Supply Chain Management Systems (SCMS) na University of Columbia, URC, USA-Presidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.*

***160.*** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na *AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, CCBRT, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT*, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, MUKIKUTE, FAWETA, TAMWA, TAWLA, TGNP, *MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT*, *Rotary Club International*, SIKIKA, *Shree Hindu Mandal*, *TANNA, TPHA, TPRI*, *Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI,*



*USADEFU, White Ribbon Alliance,* Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya.

***161.*** ***Mheshimiwa Spika,*** navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii.

***162.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza

majukumu yangu. Aidha naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu . Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara yangu. Nawashukuru pia, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, na Wakurugenzi wa Hospitali Maalum na za Rufaa za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, ya Kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

***163.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa.



Kwa wananchi na hasa wanawake wa Mkoa wa Tanga nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuendeleza Mkoa wetu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu.

## MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17

***164. Mheshimiwa Spika,*** ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka 2016/17, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya **Shilingi 166,138,358,857** kutoka katika mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu na vyanzo vya makao makuu. Aidha naomba pia Bunge lako Tukufu likubali na kuidinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake yenye jumla ya **Shilingi 845,112,920,056.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 317,752,653,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 527,360,267,056.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-**

**Fungu 52 - Afya**

**Mapato**

***165. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 163,755,679,857.00** Kati ya fedha hizo **Shilingi 146,968,868,000.00** zitakusanywa katika mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na



**Shilingi 16,786,811,875.00** ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na Mabaraza ya Kitaaluma.

**Matumizi ya Kawaida**

***166. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 277,604,173,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 58,151,377,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 219,452,796,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara **Shilingi 41,198,409,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara, Makao Makuu na **Shilingi 178,254,387,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

**Miradi ya Maendeleo**

***167. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 518,511,683,780.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo fedha za ndani ni **Shilingi 320,134,600,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 198,377,083,780.00**.

**Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mapato**

***168.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Fungu 53 inatarajia kukusanya **shilingi 2,382,679,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii, ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni

**Matumizi ya Kawaida**

***169.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 40,148,480,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 21,479,351,200** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 18,669,128,800** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

**Miradi ya Maendeleo**

***170.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 8,848,583,276** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,365,400,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,483,183,276** ni fedha za nje.



***171.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz. na www.mcdgc.go.tz.

***172.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja

**VIREFU VYA VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| AfDB | - | African Development Bank |
| AGOTA | - | Association of Gynaecologists and Obstetricians of Tanzania |
| AGPAHI | - | Ariel Glaser Paediatric Health AIDS Health Care Initiative |
| AIDS | - | Acquired Immuno-Deficiency Syndrome |
| AIHA | - | American International Health Alliance |
| AMREF | - | African Medical and Research Foundation |
| APHFTA | - | Association of Private Health Facilities in Tanzania |
| APHL | - | Association of Public Health Laboratories |
| ARV | - | Anti-Retro Viral |
| ASCP | - | American Society for Clinical Pathology |
| ASM | - | American Society for Microbiology |
| BADEA | - | Banque Arabepour Development Economique en Afrique |
| BAKWATA | - | Baraza Kuu la Waislamu Tanzania |



| | | |
|---|---|---|
| CBM | - | Christoffel Brinden Mission |
| CCBRT | - | Comprehensive Community Based Rehabilitationin Tanzania |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CCT | - | Christian Council of Tanzania |
| CDC | - | Centres for Disease Control and Prevention, Atlanta Georgia– USA |
| CHF | - | Community Health Fund |
| CLSI | - | Clinical and Laboratory Standards Institutes |
| CORDAID | - | Catholic Organization for Relief and Development Aid |
| CSSC | - | Christian Social Services Commission |
| CUAMM | - | International College for Health Cooperation in Developing Countries |
| CUHAS | - | Catholic University of Health and Allied Sciences |
| DANIDA | - | Danish International Development Agency |
| DDH | - | District Designated Hospital |
| DFATD | - | Department of Foreign Affairs, Trade and Development |

| | | |
|---|---|---|
| DFID-UK | - | Department for International Development |
| DHIS | - | District Health Information Software |
| DNA | - | Deoxyribo Nucleic Acid |
| DPT-HB | - | Diptheria, Pertussis Tetanus, Hepatitis B |
| EAC | - | East African Community |
| ECSA-HC | - | East, Central and Southern Africa Health Community |
| EED | - | Electro Encephalogram |
| EGPAF | - | Elizabeth Glaser Paediatric AIDS Foundation |
| ELCT | - | Evangelical Lutheran Church of Tanzania |
| EU | - | European Union |
| FHI | - | Family Health International |
| FINIDA | - | Finish International Development Agency |
| GAVI | - | Global Alliance for Vaccine and Immunisation |
| GE – USA | - | General Electric – United States of America |
| GIZ | - | German Society for International Cooperation (Deutsche Gesellschaftfür Internationale Zusammenarbeit) |
| GoT | - | Government of Tanzania |



| | | |
|---|---|---|
| GSF | - | Good Samaritan Foundation |
| GSK | - | Glascow SmithKline |
| HIB | - | Haemophilus Influenza Type B |
| HIV | - | Human Immuno Deficiency Virus |
| HPV | - | Human Papiloma Virus |
| IAEA | - | International Atomic Energy Agency |
| ICAP | - | International Center for AIDS Care and Treatment Programs |
| ILO | - | International Labour Organisation |
| ILS | - | Integrated Logistic System |
| IMA | - | International Missionary Association |
| IMTU | - | International Medical and Technology University |
| ISO | - | International Standard Organization |
| JICA | - | Japan International Cooperation Agency |
| KCMC | - | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| KfW | - | Kreditfeur Wiederaufbau |
| KOICA | - | Korea International Cooperation Agency |

| | | |
|---|---|---|
| MAT | - | Medical Association of Tannzania |
| Mb. | - | Mbunge |
| MDH | - | Management of Development Health |
| MDP | - | Mectizan Donation Programme |
| MDR-TB | - | Multi Drug Resistance -Tuberculosis |
| MEDA | - | Menonnites Economic Development Associates |
| MEHATA | - | Mental Health Association of Tanzania |
| MEWATA | - | Medical Women Association of Tanzania |
| MMAM | - | Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi |
| MNH | - | Muhimbili National Hospital |
| MOI | - | Muhimbili Orthopaedic Institute |
| MSD | - | Medical Stores Department |
| MSF | - | Medicine Sans Frontiers |
| MSH | - | Management Science for Health |
| MTUHA | - | Mfumowa Taarifaza Uendeshaji Huduma za Afya |
| MUKIKUTE | - | Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu – Temeke |



| | | |
|---|---|---|
| MVA | - | Manual Vacuum Aspiration |
| NACTE | - | National Accreditation Council for Technical Education |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund |
| NIMR | - | National Institute of Medical Research |
| NORAD | - | Norwegian Agency for Development |
| NSSF | - | National Social Security Fund |
| ORCI | - | Ocean Road Cancer Institute |
| ORET | - | Overseas Related Export Trade |
| P4P | - | Pay for Performance |
| P4H | - | Providing for Health |
| PASADA | - | Pastoral Activities and Services for People with AIDS |
| PAT | - | Paediatric Association of Tanzania |
| PEPFAR | - | President’s Emergency Plan for AIDS Relief |
| PHC/PHCI | - | Primary Health Care/Primary Health Care Institute |
| PRINMAT | - | Private Nurses and Midwives Association of Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| PSI | - | Population Service International |
| RTI | - | Research Triangle Institute |
| SADC | - | Southern Africa Development Cooperation |
| SADCAS | - | Taasisi ya Idhibati ya Nchi za SADC |
| SAREC | - | Swedish Agency for Research Cooperation in Development Countries |
| SCMS | - | Supply Chain Management System |
| SDC | - | Swiss Agency for Development and Cooperation |
| SIDA | - | Swedish International Development Authority |
| TANESA | - | Tanzania Netherlands Support to AIDS Control |
| TEC | - | Tanzania Episcopal Conference |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THPS | - | Tanzania Health Promotion Support |
| TISS | - | Tanzania Interbank Settlement Systems |
| TPHA | - | Tanzania Public Health Association |
| TPRI | - | Tanzania Pesticides Research Institute |
| UKIMWI | - | Upungufu wa Kinga Mwilini |



| | | |
|---|---|---|
| UN | - | United Nations |
| UNAIDS | - | United Nations Programme on AIDS |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
